# Nipashe

Jumatatu Aprili 22, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579898

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Agizo la JPM ujenzi wa stendi kaa la moto Njombe

UKURASA 5


Nipashe Spotik

NIPASHE JUMATATU APRILI 22, 2019

WAS WA KUPOTEA, KUTAKATA KUREJEA KWA ZIDANE MADRID UK.16

ISIKUPITE

Cristiano Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza kutwaa ubingwa katika ligi tatu kubwa barani Ulaya, Serie A, La Liga na Premier League. Msimu huu amekuwa nguzo muhimu kwa Juventus kutwaa taji la Ligi Kuu Italia kwa kufunga mabao 19 katika mechi 27 alizocheza hadi sasa.

MSHIKEMSHIKE...

Cristiano Ronaldo akipata upinzani mkali kutoka kwa mabeki wa Fiorentina katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Allianz juzi na wao kushinda 2-1, kwa ushindi huo Juventus ikatwaa rasmi ubingwa huo, hiyo ikiwa ni mara ya nane mfululizo.

HABARI UK. 30

UKURASA 13

# Askofu ataka haki uchaguzi wa mitaa

• **Asema** ndio msingi uchaguzi mkuu, wengine waonya rushwa... *Endelea ukurasa 2&3*



Baadhi ya waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), wakishiriki ibada ya Pasaka iliyofanyika Kanisa Kuu la Usharika wa Dodoma Mjini, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSPEH**

## Anna Henga: Naamini 50/50 inawezekana katika uongozi

UKURASA 4






## H/shauri zabainika kuwaficha wanufaika mikopo elimu juu

UKURASA 5

# Serikali yapewa neno elimu bora

**Na Waandishi Wetu**

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), limetoa ujumbe mzito kwenye sekta ya elimu huku likieleza kuwa kubadilishwa kwa sera na miongozo ya elimu ni ishara ya wazi kwamba Watanzania bado hawajui wanachokitaka.

Askofu wa Jimbo Katoliki la Kayanga, Mhashamu Almachius Rweyongeza, alisoma jana ujumbe huo wa TEC ambao ndani yake ulianishwa mambo saba yanayotakiwa kufanyiwa kazi na serikali.

Ujumbe huo ulisomwa katika misa ya kitaifa iliyofanyika Kanisa la Mtakatifu George jimbo katoliki la Kayanga ambapo Askofu Rweyongeza alisema sekta hiyo bado kama taifa halijajua rasilimali watu wawe na sifa gani, hawajui wanataka taifa la leo na kesho liweje.

"Mwelekeo wetu ni upi?...kila mara tunashuhudia mitaala ya elimu inabadilishwa bila kufanyiwa utafiti wa kina na kujidhihirisha kwa maslahi mapana kwa mushtakabali wa taifa," alisema.

Alisema baada ya taifa kupata uhuru, Mwalimu Julius Nyerere aliwabaini maadui watatu wa amani, maendeleo na ustawi wa taifa kuwa ni ujinga, maradhi na umaskini.

"Hatutafurahia uhuru kama hawa maadui watatu ujinga, maradhi na umaskini wanatuchachafya, kwenye geti la chuo fulani yapo maandishi nayanukuu, 'Ukitaka

INAENDELEA UK.8

# Paroko: Tusiogope kuitwa wadhaifu kwenye maisha

**Na Salome Kitomari**

WATANZANIA wametakiwa kutoogopa kuitwa dhaifu pale wanaoshindwa kuishi maisha yanayompendeza Mungu, badala yake kujikweza na kuonea wengine.

Akihubiri katika mkesha wa Pasaka, Paroko wa Parokia ya Mtakatifu Augustino, Salasala, jijini Dar es Salaam, Padri Peter Asenga, alisema mtu kuitwa dhaifu siyo kosa kwa kuwa inatokana na matendo yake ambayo wakati mwingine yanakwaza wengine.

Alisema binadamu mwenye kiburi kujikweza, kujiona bora kuliko wengine, anayeonea wengine ni ambaye hayaishi maisha ya imani na fumbo la kufufuka kwa Yesu huyo ni dhaifu.

"Usiogope kuitwa dhaifu kwa kuwa ukiwa na mambo hayo ni lazima utaitwa dhaifu, mnatakiwa kuacha njia mbaya na kuishi maisha ya imani na ndipo udhaifu hautakuwepo," alisema Padri Asenga.

Aidha, alisema ni vyema waumini wakaacha masengenyo na kuwanyooshea vidole wengine, bali wanapoingia katika fumbo la Pasaka waonyeshe mabadiliko.

Akihubiri katika ibada ya Pasaka jana, alisema maisha ya kiristo yalikuwa ya matendo mema na huruma ambayo yanapaswa kuigwa na watu wote katika kuishi na wanadamu wengine.

Alisema kanisa limejikita katika kuboresha huduma za kijamii kwa kushirikiana na serikali kwa kuwa linajua umuhimu wa kumuhudumia binadamu kimwili na kiroho. "Kanisa linajenga hospitali kwa ajili ya kunusuru wagonjwa wanaotaabika kwa magonjwa, linajenga shule ili kuwaendeleza watu kielimu kwa faida ya sasa na baadaye," alisema.

Aidha, alisema matendo ya huruma yanapaswa kuwa endelevu kwa maisha ya kila siku ili kuwajali wahitaji na wenye shida mbalimbali ikiwamo kuondokana na umaskini.

"Itapendeza sana ikiwa kila mmoja ataendeleza matendo ya huruma kwa kutoa mchango kwa mtu mmoja moja ambao utasaidia taifa kwa ujumla. Matendo hayo yaanzie katika mazingira tunayoishi, kazini na kokote kwa kila mmoja kuwajibika ipasavyo," alisema.



# Askofu ataka haki uc

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Masasi mkoani Mtwara, Dk. Jemsi Almasi, amewataka viongozi wanaosimamia haki nchini kutimiza wajibu wao ili kuepusha taifa kuingia katika mifarakano itakayo sababisha viasharia vya uvunjifu wa amani na kulikosesha taifa utulivu wa amani.

Aliyasema hayo jana katika ibada ya Pasaka mjini Masasi katika Kanisa Kuu la Baltamayo Mtume na Mariam Mbarikiwa.

Alisema taifa hili limebahatika kupata viongozi waadilifu ambao wameendelea kudumisha amani kwa kutenda haki, hivyo wasijitokeze wachache ambao watataka kuonyesha nguvu ya nafasi zao katika kuliongoza taifa kwa kutaka kufarakanisha jamii kwa sababu ya maslahi yao

Askofu Dk. Almasi alisema mifarakano ambayo imekuwa ikijitokeza nchini na katika nchi kadhaa zikiwamo za jirani mara kadhaa imekuwa ikisababishwa na viongozi wachache wanaosimamia haki kupitia nafasi zao, ambao wamekosa uadilifu wa kusimamia haki.

Aidha alisema sehemu yoyote yenye mifarakano, chuki na unyanyasaji ukiwamo ubaguzi ni wazi sehemu kama hiyo haitakuwa na upendo na amani, na mwisho wa siku nchi huingia kwenye machafuko ya vita ambavyo husababisha kinamama na watoto kuathirika pasipo na

# Mkuu KKKT ashangaa kasi ndoa kikristo kuvunjika

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amesema kanisa bado linajiuliza ni kwa nini ndoa nyingi za kikristo zinavunjika kuliko wakati mwingine wowote, huku akieleza chanzo cha kuvurugika kwa ndoa hizo ni watu kushindwa kuzingatia ahadi na mapatano waliyowekeana mbele za Mungu.

Alisema chanzo kikubwa cha migogoro hiyo kushamiri nchini ni kushindwa kutekelezwa kwa mapatano kati ya wawili wanaofunga ndoa na ikiwa Watanzania wanataka kudumu katika ndoa hizo ni lazima mapatano hayo yaheshimiwe.

Askofu Dk. Shoo alikuwa akizungumza jana katika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini, wakati akihubiri katika ibada ya Sikuu ya Pasaka.

"Chanzo cha talaka ni kudhoofika kwa misingi ya familia na kutozingatia ahadi walizopeana, siku hizi watu wengi hawazipi umuhimu zile ahadi wanazopeana wakati wa kuoana, wanazichukulia kama jambo jepesi na kuzingatia sherehe na mavazi. Ipo haja kwa viongozi wa dini, familia na jamii kulitazama suala hilo kwa jicho pana ili uwepo muda wa kutosha wa kuwashauri wale wanaotaka kuingia kwenye ndoa.

Mwaka jana peke yake katika Manispaa ya Moshi kulikuwa na maombi ya talaka 27, jambo ambalo linaelezwa kuwa limeathiri idadi kubwa ya watoto kuumia kisaikolojia na kiakili kwa kiasi kikubwa, baada ya talaka hizo kutolewa kutokana na baadhi ya wazazi kupunguza malezi kwao.

Pia, Askofu alitaja athari zitakazojitokeza kama Wakristo na Watanzania hawatatembea na Mungu kuwa ni ubabe, chuki, visasi, kutovumiliana, kutoheshimiana na hatimaye kusambaratika kwa uhusiano mwema na Mungu.



Waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Azania Front jijini Dar es Salaam, wakiwa katika ibada ya Pasaka jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Maaskofu walia rushwa

**Na Waandishi Wetu**

MAASKOFU wamekemea vitendo vya rushwa ambavyo wamedai kufanywa na matumishi wa serikali hali inayokwamishwa ufanisi kazini na kuwanyima haki Watanzania.

Wameeleza kuwa hivi sasa rushwa imetawala hadi katika mahakama na kudai hata mawakili ambao ndio watetezi wa wanyonge wanapokea rushwa.

Wakihubiri katika makanisa mbalimbali katika ibada ya Pasaka, maaskofu hao kutoka makanisa ya Anglikana, Katoliki, wamesema hali hiyo kama haitapigwa vita na watu wote ni dhahiri kuwa wanyonge hawatapata haki zao.

Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Kati, Dk. Dickson Chilongani, amesema licha ya serikali kupambana na rushwa, hali hiyo bado ipo kwenye ofisi za umma.

Akihubiri katika Kanisa Kuu la Anglikana jijini hapo, Dk. Chilongani alisema ni aibu kwa watumishi wa serikali kuendekeza vitendo vya rushwa na ufisadi.

Alisema kwa sasa rushwa zinaendelea kufanyika katika ofisi za umma huku jina linalotumika kuidai likibatizwa kama 'support document'.

"Hivi karibuni nilisafiri kwenda nje ya nchi cha kusikitisha nilipofika uwanja wa ndege wa Dar es Salaam, nilipokelewa na wahudumu ambao ni watumishi wa serikali licha ya kuwa sikuwaomba msaada wowote wa kunisindikiza au kufunga zipu ya begi langu, lakini waliniomba hela ya soda ambayo ni rushwa," alisema Askofu Dk. Chilongani.

Alitahadharisha vita ya rushwa isiwe ya mtu mmoja au serikali pekee bali iwe ya Watanzania wote na kama haitapigwa vita na watu wote ni dhahiri kuwa wanyonge hawatapata haki zao.

Aidha, alikemea baadhi ya askari polisi ambao wanaendekeza vitendo hivyo.

"Rushwa haikuanza leo, imekuwapo kwa muda mrefu hata kipindi cha Yesu, Yuda alihongwa vipande 30 ili amsaliti Yesu na akafanya hivyo, haikutosha wakati Yesu yupo kaburini alipofufuka askari walihongwa ili waseme Yesu hakufufuka bali ameibiwa jambo ambalo dhahiri lilionekana kuwa ni kupotosha ukweli," alisema.

Aliwataka waumini wa kanisa hilo kuwafikia watu wenye uhitaji badala ya kutumia sikukuu kufanya anasa ikiwamo ulevi na uzinzi.

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Zanzibar, Augostino Shao, alisema pamoja na juhudi zote za rais za kuhimiza uwajibikaji na kukemea ubadhirifu wa mali ya umma, yeye mwenyewe amekiri bado rushwa ni kubwa.

Akihubiri katika ibada ya Pasaka Kanisa la Minara miwili Shangani, mjini hapo, alisema ushindi wa Kristo dhidi ya dhambi ni kwa sababu alitaka kujenga haki kwa wote na kwamba wanadamu wote ni sawa na wanastahiki heshima.

Alieleza kuwa hivi sasa rushwa imetawala

INAENDELEA UK. 8

# haguzi wa mitaa

hatia.

"Viongozi wote wa dini hapa nchini tunahubiri upendo na amani na ndio maana taifa limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu tunaheshimu katiba ya nchi, ambayo ni sheria mama na msingi wa taifa hili,"alisema Dt. Almasi

Alisema kama viongozi wanaosimamia haki nchini wakitenda haki kama vitabu vya dini na katiba ya nchi inavyotaka, ni wazi kuwa muendelezo wa amani na upendo utadumu zaidi, lakini kama watapindisha haki, basi wataendeleza uwapo wa mifarakano na machufuko.

Alisema hivi karibu taifa litaingia kwenye uchaguzi wa serikali wa mitaa ambao ndio msingi wa uchaguzi kuu wa mwaka 2020, hivyo wanaomba uchaguzi huo uwe wa haki na asitokee kiongozi yeyote mwenye mamlaka akapindisha haki na kusababisha malalamiko ya uonevu.

Askofu huyo aliongeza kuwa kama uchaguzi wa serikali za mitaa usipofanyika kwa haki na uhuru, hata uchaguzi kuu unaweza ukavurugika kwa sababu ya mifarakano ya uchaguzi wa serikali za mitaa.

# TEC yataka mikakati madhubuti bima afya

**Na Waandishi Wetu**

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), limeiomba serikali kuweka mikakati madhubuti ya kifedha na utaratibu wa kuchangia bima afya kwa watu ambao hawana uwezo wa kupata huduma hiyo waweze kuipata.

Akisoma ujumbe wa Pasaka uliotolewa na TEC kwenye ibada ya Pasaka kitaifa katika Kanisa la Mtakatifu George Jimbo Katoliki la Kayanga wilayani Karagwe mkoani Kagera, Askofu Almachius Rweyongeza alisema kuna idadi kubwa ya Watanzania ambao ni maskini na wameshindwa kupata huduma hiyo.

"Pia tunaiomba serikali iweke mikakati madhubuti ya kifedha, na utaratibu wa kuchangia na hatimaye upatikanaji wa huduma za afya kwa watu ambao hawana uwezo kujigharamia huduma za afya uwe mwepesi," alisema Askofu Rweyongeza.

Alisema TEC inatambua juhudi za serikali za kuweka mfumo wa bima ya afya jumuishi unaolenga kumfikia kila mwananchi

Askofu Rweyongeza alisema kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), asilimia 28 ya Watanzania ambao ni sawa na milioni 14.2, ni maskini kabisa.

"Hivyo basi idadi hiyo hawana uwezo kabisa wa kujilipia bima kugharamia huduma za afya. Kwa mantiki hii kama taifa tunalo jukumu la kuhakikisha wananchi hawa maskini wanawezeshwa kupata huduma bora za afya kote nchini."

Alisema kanisa kama sehemu ya jamii wanayo wajibu wa kuhakikisha wanahimiza

INAENDELEA UK. 8




# Anna Henga - Apata tuzo mwanamke jasiri

## ■Anaamini 50/50 katika uongozi inawezekana

**Na Salome Kitomari**

MACHI 7, mwaka huu kulifanyika hafla ya kutoa tuzo kwa wanawake 10 jasiri duniani (wenye uthubutu) wa kuleta mabadiliko chanya katika jamii zao (International Women of Courage Award), 2019.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga (pichani), kutoka Tanzania alikuwa miongoni mwa wanawake hao waliotunukiwa tuzo hiyo na Serikali ya Marekani. Tunzo hiyo hutolewa kila mwaka.

Hafla ya kukabidhi tuzo hizo ilihudhuriwa na Mke wa Rais wa Marekani, Melania Trump, na wengine waliotunukiwa ni kutoka nchi za Bangladesh, Burma, Djibouti, Misri, Jordan, Ireland, Montenegro, Peru na Sri Lanka.

Tunzo hiyo ilianzishwa mwaka 2007 kutambua mchango wa wanawake wanaojitoa kwa nguvu na ujasiri kama viongozi katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii zao bila kujali hatari ya maisha ya binafsi.

Mpaka sasa kupitia tuzo hiyo, Ikulu ya Marekani imetambua mchango wa wanawake zaidi ya 120 kutoka nchi 65 katika kutetea haki za binadamu, kudumisha nafasi ya wanawake katika jamii na kudumisha amani na utawala bora katika nchi zao.

Nipashe ilifanya mahojiano maalum na Mkurugenzi huyo na yalikuwa kama ifuatavyo:

**Swali:** Tuzo ya Mwanamke jasiri ina maana gani:

**Henga:** Nimepata tuzo kutoka Serikali ya Marekani, wao wenyewe wanaangalia katika wanaAzaki, serikalini na sehemu mbalimbali mwanamke anayeonekana ana ujasiri wa kufanya vitu ambavyo vinaleta mabadiliko chanya katika jamii hasa kwenye haki za wanawake.

Ubalozi wa Marekani nchini ulipendekeza jina langu, nimekuja kujua nimeshatangazwa na kuambiwa natakiwa kwenda Marekani na tulikutana wanawake 10.

**Swali:** Ni kitu gani hasa umekifanya hadi kimekupa tuzo hii?

**Henga:** Kwanza kabisa ni kufanya vitu ambavyo vinahatarisha maisha yako, unahatarisha familia na shirika unalofanyia kazi, kwa walivyoangalia kwangu ni kutokana na muktadha wa sasa nchini wa kisiasa na kijamii, kuendelea kutetea haki za watu bila kujali mazingira ni jambo kubwa sana.

Pia, tulishafanya mradi mkubwa wa masuala ya ukeketaji Serengeti ambao ulihatarisha maisha kwani ilifikia mahali tukaenda kumkamata mtuhumiwa tukiwa na polisi.

**Swali:** Mlifanyaje hadi kumkamata mtu huyo?

**Henga:** Polisi walituambia ni



hatari sana kwa kuwa nyie ni raia, lakini sisi ilikuwa lazima tukamuonyesha askari kuwa nyumba ni ile kule, ilibidi tuhame hoteli na kuondoka kwenye mji huo kwa haraka ili kuepusha jambo lolote baya kutukumba. Nadhani hii ilichangia kuwa nimefanya kitu cha ujasiri.

Kitu kingine ni wakati wa kutoa elimu ya Katiba mpya ambayo tulisisitiza uwapo ushiriki wa wanawake 50 kwa 50 na kutaka Katiba iseme hivyo, na ilifanya hivyo na Katiba Pendekezwa ilibeba suala la wanawake vizuri.

Tulifurahi kwa kuwa Katiba ilitambua suala la jinsia na kulipa nafasi, lakini pia tulizunguka wilaya kwa wilaya, kata kwa kata kuwafikia wananchi kuwapa elimu ya Katiba na walishiriki vyema kutoa maoni yao.

Kingine walichokiona, ni wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, tuliwafundisha wanawake kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali.

Tuliwatafuta kupitia vyama vya siasa na wengi walitangaza nia ya kugombea na wakawa wagombea na tukawafundisha namna ya kufanya kampeni, jinsi ya kuongea mbele za watu na kuwashawishi watu kukubaliana na hoja zako.

Tulipata wengi sana walioshinda kwenye nafasi za udiwani na wabunge wachache, kwenye ubunge hatukufanikiwa sana kutokana na mfumo dume, hali ya kiuchumi ambao unamtaka kuwa na fedha nyingi, lakini hata kutangaza nia ni ujasiri wa hali ya juu ambao tunajua hata akikosa wakati mwingine atagombea.

**Swali:** Jamii bado inakabiliwa na matatizo ya ukatili, mfano hivi karibuni kulikuwa na matukio ya watoto kupotea, ukeketaji wa wanawake na watoto, mimba za utotoni na ndoa za utotoni. Je nini kifanyike ili kumaliza matatizo haya?

**Henga:** Kwanza wavunjaji wa haki wapelekwe kwenye vyombo vya sheria na jamii ihusike kutoa ushahidi ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Lakini tufanye utafiti ni kwanini mambo haya bado yanatokea, kwa sababu unaweza ukafunga kijiji kizima na wakatoka wakaendelea.

Timu ya watafiti ilivyokwenda Simiyu na Njombe, waligundua mauaji ya watoto yalikuwapo toka zamani, lakini siyo kwa kiwango kikubwa kama wakati huu ambako watoto 10 waliuawa na kunyofolewa viungo mbalimbali.

Walibaini kuwa chanzo chake ni imani za kishirikina, wanaamini wakiwa na sikio au mguu wa mtoto utapata utajiri, na kingine ni roho ya visasi kwa wazazi waliogombana ambao huua mjukuu au mtoto.

Tulifikiri utoaji wa elimu ni muhimu sana kuwaambia kuwa sikio au kiungo cha mtoto hakina uhusiano na mafanikio yake, kinachotakiwa ni kufanyakazi kwa bidii, waweke malengo na tuwatafutie masoko na kutangaza biashara zao na siyo viungo vya watoto.

**Swali:** Kwa mtazamo wako 50 kwa 50 inawezekana Tanzania?

**Henga:** Inawezekana kwa kuwa tulikotoka ni mbali yaani asilimia tano kwenye uchaguzi wa vyama vingi hadi sasa ni hatua kubwa, Zanzibar wameshafikia asilimia 40 nasi tunaelekea 40, hivyo inawezekana, lakini lazima tufanye kazi kubwa sana.

Kwanza ni lazima kubadilisha mtazamo wa jamii, na kaulimbiu ya mwaka huu ni badilisha mtizamo kwasababu mwanamke anaweza kuwa kiongozi au mtu yeyote.

Wapigakura wanatakiwa wasimwangalie mwanamke kwa jinsia yake bali wamwagalie kama mtu kutokana na sifa zake, ukiangalia nchi za wenzetu mtu anaangaliwa kama mtu, lakini kwenye jamii zetu wanamwangalia kama ni mwanamke au mwanamume.

Kwenye kampeni wagombea wanawake walieleza changamoto wanazokutana nazo za maswali kama hivi ameolewa, ana watoto au ana mume, lakini mwanamume hawaangalii vyote hivyo bali uwezo wake wa kuongoza.

Bado kuna kazi kubwa sana ya kufanya na ni lazima tushirikiane na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), kutoa elimu kwa wapigakura ili wamwangalie mtu kama mtu na sifa alizonazo na siyo jinsia yake.

Aidha, tunatakiwa kuongeza nguvu kwenye kuwaandaa wanawake kugombea nafasi mbalimbali, ili tuwe na madiwani, wabunge wengi wanawake.

**Swali:** Je inawezekana kubadili fikra za wapiga kura na kumwamini mwanamke?

**Henga:** Inawezekana kwa kuwa muda tunao wa kutosha, tuanze kwenye vyama na wagombea wenyewe kuvaa mwili wa sponji na kutosikiliza maneno yanayorushwa kwake kwa kuwa wapo wanawake waliogombea na wameshika nafasi hizo katika mazingira yaliyopo.

Kubadilisha fikra itachukua muda mrefu, lakini itafikia wakati idadi ya wanawake wenye uwezo katika meza ya maamuzi wataongezeka.

Idadi ya wanawake kwenye teuzi mbalimbali imeshuka, na wengi wanaoteuliwa ni wasomi wenye udaktari wa filosofia na Profesa, ngazi ambazo bado hazina wanawake wengi kutokana na misingi iliyojengwa miaka mingi.

Tunaelekea kuwa na madaktari wengi, lakini bado hatujaweza kufikia katika muktadha wa kijamii, lakini kwa kuangalia wasomi tutakuwa wachache, lakini nafasi kama za uongozi wa Bodi, wakuu wa mikoa na wilaya anaondolewa mwanamke na kupewa mwanamume na hivyo kuzidi kupunguza idadi ya wanawake kwenye nafasi za uongozi.

Inawezekana mfumo wa rais kupelekewa majina huenda inapita katika mikono yenye macho ya kisiasa ambayo bado wapo wanaume wengi, lakini likiangaliwa kitaaluma kuna wanawake wengi wenye uwezo wa kuongoza.

Henga anasema upo msemi kuwa wanawake hawapendani, kwamba ni wengi sana, lakini hawawachagui wanawake wenzao na kama wangependana wangeweka rais madarakani.

Anasema mfumo uliokuwapo ulimfanya mwanamke aonekane kama siyo kitu na wataalamu wa saikolojia wanasema ukijipenda wewe utampenda na mwenzako na ukijithamini wewe utamthamini na mwenzako.

Mwanamke amekuzwa katika mazingira ya kutojithamini na ndiyo maana anapokwenda kwenye sanduku la kura haoni kama mwanamke anaweza kuwa kiongozi.

Mfano, mimi natokea usukumani ambako mwanamke ni daraja la pili na kuna misemo kuwa mwanamke hakuwagi yeye yupo daraja la chini, hivyo mwanamke aliyeambiwa hivi hawezi kugombea na atahitaji elimu ya kubadili fikra kwa kuwa yeye mwenyewe haamini kuwa anaweza kuwa kiongozi hivyo hawezi kumwamini mwanamke mwenzie.

Henga anasema anatamani angekuwa na fedha zote duniani ili azunguke kila kijiji, kata na wilaya ili aongee na wananchi wabadili mtizamo hasi dhidi ya mwanamke.

## HABARI KITAIFA



Afisa mizani akirekebisha mzani wake kabla ya kupima uzito wa magari yaliyokuwa yanapita katika mitaa ya Tandika Mwembe Yanga wilayani Temeke jijini Dar es Salaam. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Halmashauri zabainika kuwaficha wanufaika mikopo elimu ya juu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini baadhi ya halmashauri zimekiuka sheria kwa kutoitaarifu Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kuhusu kuajiri watumishi ambao ni wanufaika wa wa mikopo inayoitoa.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18, CAG Assad anasema Kifungu cha 19 ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Mwaka 2004, kama ilivyorekebishwa mwaka 2016, inahitaji kwa lengo la kuwatambua wanufaika wa mikopo hiyo, kila mwajiri kuiarifu bodi kuhusu ajira ya mtu yeyote ambaye ana shahada au stashahada, ndani ya siku 28 kutoka tarehe ambayo mtu huyo ameajiriwa.

"Nilipitia mfumo wa mishahara, mafaili binafsi na orodha ya wanufaika wa HESLB wasiorejesha mikopo yao katika mamlaka za serikali za mitaa 6 na kugundua kwamba, mikopo ya elimu ya juu kwa watumishi 21 ya jumla ya Sh. 269,913,969 (Sh. milioni 269.914) katika mamlaka za serikali za mitaa mbili haikurejeshwa kwa sababu mamlaka zilishindwa kuiarifu bodi juu ya uwapo wa wanufaika kama inavyotakiwa na sheria yake," Prof. Assad anabanisha.

"Pia nilibaini kuwapo kwa mamlaka za serikali za mitaa nne ambazo hazikuitaarifu HESLB juu ya uwapo wa wanufaika wa mikopo hiyo kwa watumishi wao kama inavyohitaji Sheria ya Bodi ya Mwaka 2004 katika kipengele cha 19."

Kwa mujibu wa CAG Assad, halmashauri ambazo hazikutoa taarifa kwa HESLB ni Geita ambayo ina watumishi 257, Ikungi yenye watumishi saba wanaotakiwa kurejesha Sh. milioni 113.143, Songwe iliyo na wanufaika 14 wanaotakiwa kurejesha Sh. milioni 156.771 na Manyoni yenye watumishi wawili.

Katika ripoti hiyo, Prof. Assad pia anabainisha kuwa Halmashauri za Mbulu na Mkuranga nazo ni miongoni mwa mamlaka ambazo hazijatoa taarifa kwa HESLB kuhusu uwapo wa wanufaika wa mikopo ya bodi hiyo ambao hawajaanza kurejesha mikopo. "Kwa mtazamo wangu, hali hii imesababishwa na upungufu katika idara ya rasilimali watu katika kutambua watumishi wanufaika kwa lengo la kuitaarifu HESLB kama kifungu cha 19 cha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya mwaka 2004 kinavyotaka.

"Kutokutolewa kwa taarifa kunaweza kuwa kikwazo katika kurejesha mikopo hiyo, hivyo kutaathiri malengo ya HESLB ya kutoa mikopo ya kutosha kwa wanafunzi zaidi wa elimu ya juu wenye uhitaji.

"Napendekeza kwa uongozi wa mamlaka za serikali za mitaa kupanga namna ya kufanya marejesho ya mikopo ya wafanyakazi walionufaika nayo na kuchukua hatua mwafaka kutambua wanufaika wa mikopo hiyo ambao bado hawajaanza kufanya marejesho, na kuitaarifu HESLB," Prof. Assad anashauri katika ripoti yake hiyo.

HESLB ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya Mwaka 2004, ikiwa na mamlaka ya utoaji wa elimu ya kwa njia ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wanaosoma vyuo vinavyotambulika. Pia, ina mamlaka ya kukusanya na kurejesha fedha zote zinazodaiwa kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo.

# Agizo la JPM ujenzi wa stendi kaa la moto Njombe

**Na Waandishi Wetu,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji wa Njombe Wilaya ya Njombe mkoani humo, imeonyesha kuwa haitaweza kutekeleza agizo la Rais John Magufuli kwa kukamilisha ujenzi wa stendo ya mabasi ndani ya siku 30.

Rais Magufuli akiwa ziarani mkoani Njombe alipokea malalamiko ya wananchi kuhusiana na kuchelewa kukamilika kwa stendi hiyo, hivyo kutoa siku 30 iwe imekamilika kuanzia Aprili 10.

Hata hivyo, zikiwa zimepita siku takribani 10 baada ya Rais Magufuli kutoa muda huo, halmashauri hiyo imeingiwa na shaka kama itaweza kutekeleza agizo hilo.

Aliyetoa kauli ya kuonyesha shaka hiyo, huku akieleza kuwa hali hiyo inatokana na vikwazo kadhaa ni MwenyekitI wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Edwin Mwanzinga, ambaye amesema ujenzi huo hauwezi kukamilika kwa asilimia 100 ndani ya muda huo kutokana na ukubwa wa kazi iliyo mbele yao.

Siku ambayo Rais Magufuli alitoa agizo hilo, alieleza kushangazwa na ujenzi wa stendi hiyo kutokamilika licha ya fedha za utekelezaji kutolewa zote.

**CHANGAMOTO**

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti Mwanzinga alisema sababu kubwa inayowakwamisha makandarasi kushindwa kukamilisha kazi hiyo kwa muda uliotolewa na

INAENDELEA UK. 8

Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-

- Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=
- Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=
- Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima
- Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku



# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Serengeti Boys isitelekezwe, benchi la ufundi limulikwe

**JUMAPILI** wiki hii fainali za Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wenye umri chini ya miaka 17 (Afcon U-17) inayoendelea nchini, zitafikia ukingoni huku Tanzania ikiaga mapema.

Michuano hiyo iliyokuwa imepangwa makundi mawili, Tanzania, Serengeti Boys ilikuwa Kundi A pamoja na Angola, Uganda na Nigeria.

Katika michuano hiyo timu ya kwanza na ya pili kutoka Kila kundi zimekata tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia U-17 nchini Brazil Oktoba mwaka huu, ambazo ni Nigeria na Angola kutoka Kundi A na Cameroon na Guinea kutoka Kundi B.

Na kwa upande wa Serengeti Boys ambayo kushindwa kwake kufuzu fainali hizo kulitokana na kupoteza mechi zake mbili za awali dhidi ya Nigeria na Uganda, imeungana na Waganda hao pamoja na Morocco na Senegal kutoka Kundi B kuaga mapema michuano hiyo.

Wawakilishi hao wa Tanzania pamoja na wenyeji wao kwenye fainali hizo walianza kwa kipigo cha mabao 5-4 kutoka kwa Nigeria kisha wakalala 3-0 dhidi ya Uganda, kabla ya kuangukia pua mechi yao ya mwisho kwa kuchapwa 4-2 na Angola.

Kwa ujumla hatupaswi kuilaumu Serengeti Boys kwa matokeo iliyoyapata katika michuano hiyo licha ya maandalizi ya muda mrefu iliyoyafanya.

Nipashe tunakiri kwa ukongwe wa wadau wetu katika sekta ya michezo nchini, Serengeti Boys inakuwa timu ya Taifa ya kwanza ya Tanzania kuwahi kuandaliwa kwa muda mrefu tena ikipata mechi nyingi za kiwango cha juu za kujipima uwezo na kucheza mashindano mengi ya kimataifa kuelekea michuano iliyokuwa mbele yao.

Pamoja na kwamba Serengeti Boys ilikutana na timu bora katika fainali hizo, tutakosea kama tukisema kilichoiangusha ni maandalizi ya kutosha.

Yanaweza yakawa maandalizi, lakini ni kwa upande wa udhaifu wa benchi la ufundi kutokuwa na uwezo ama uzoefu wa kutosha katika kuwapa wachezaji mbinu za kutosha kulingana na mechi zilizokuwa mbele yao ama aina ya timu wanayokutana nayo.

Tunakumbuka Serengeti Boys hii hii ilipata mafanikio makubwa wakati Kim Paulsen akiwa miongoni mwa makocha waliokuwa wakiunda benchi la ufundi na kama timu ilicheza soka la kiwango cha juu na kupata mafanikio ya kuvutia.

Si lengo letu kubeza ama kudharau uwezo wa benchi la ufundi la sasa chini ya Oscar Mirambo, la hasha, bali kama wadau namba moja wa michezo nchini, tunaona alipoifikisha ni pazuri ila anahitaji ama kuongezewa nguvu au ikilazimu kupisha kabisa kocha mwenye uwezo zaidi.

Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba kwa namna Serengeti Boys ilivyoonekana ikicheza makosa ni yale yale yalikuwa yakijirudia katika kila mechi kuanzia kwa golikipa hadi washambuliaji. Hiyo inaonyesha kocha Mirambo anahitaji mshauri mzuri zaidi ama hata mwenye uwezo na uzoefu kumshinda kama ilivyokuwa kwa Paulsen


Hili si suala la Shirikisho la Soka nchini (TFF), kulifanyia mzaha ama majaribio kwani hatuwezi kuwa na timu ya Taifa bora ya wakubwa kama hakutakuwa na msingi imara hususan kwa kuwapa mbinu na ufundi vijana hawa wa Serengeti Boys.

Na katika hilo, kushindwa kufuzu Kombe la Dunia isiwe mwanzo kwa TFF kuiacha Serengeti Boys ikiparaganyika bali huu uwe mwanzo wa kuijenga kwa kuiboresha kuanzia hapo kwa kumulika wachezaji hadi benchi la ufundi.

Aidha, umefika wakati sasa wa kutafuta wachezaji wenye sifa kweli na kuacha kuchagua wachezaji wanaounda kikosi hicho kutokana na undugu ama kujuana kwa kuwa hilo nalo ni suala ambalo kwa muda mrefu limekuwa likipeleka mafanikio yetu kisoka kaburini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Serengeti Boys wapewe muda wakiendelea kujifunza zaidi

**WENYEJI,** Tanzania wametolewa kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa vijana chini ya umri wa miaka 17 (Afcon U-17), kwa kupoteza mechi zote tatu, baada ya Serengeti Boys kufungwa mabao 4-2 Jumamosi iliyopita na Angola katika mchezo wa mwisho wa Kundi A uliopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Bahati mbaya zaidi hata jirani zao, Uganda nao wametupwa nje baada ya sare ya bao 1-1 na Nigeria katika mchezo mwingine wa mwisho wa Kundi A uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam pia.

Maana yake, Nigeria iliyomaliza kileleni mwa kundi kwa pointi zake saba inaungana na Angola iliyomaliza na pointi sita kwenda nusu fainali na pia kujikatia tiketi ya fainali za Kombe la Dunia Oktoba mwaka huu nchini Brazil.

Ni ukweli mchungu kwa Watanzania na nchi za Afrika Mashariki na Kati, Ukanda wa Cecafa.

Awali, Watanzania walikuwa na matumaini makubwa si tu kupata tiketi ya kucheza Kombe la Dunia kwa vijana nchini Brazil, bali pia hata kulitwaa kombe hilo la Afcon U-17.

Maandalizi kababme ambayo Tanzania imefanya pamoja na kuiandaa vema timu ya vijana, ikichagizwa na hamasa kubwa iliyokuwapo kwa sasa nchini, lakini kwa bahati mbaya sana waswahili wanasema 'jitihada hazishindi kudura.'

Serengeti Boys hii hii ambayo inafanya vizuri ikiwa ugenini kiasi cha kutwaa makombe na kurejea nayo, imeshindwa kuwapa furaha Watanzania mbele ya mashabiki wao.

Kuna rafiki yangu mmoja huwa ananiambia mara nyingi msiba wa 'mswahili' haukosi sababu, basi wapo baadhi ya Wabongo wataongea mambo mengi kuhusu kutolewa kwa Serengeti Boys, lakini inafika wakati inabidi tukubali tu kuwa timu yetu ni bora, lakini ilikutana na timu bora zaidi. Hakuna mchawi kwenye hili.

Tuwapongeze vijana wetu hapa walipofikia na badala ya kuanza lawama, tuwape moyo ili waweze kuiwakilisha vema bendera ya Tanzania kwenye michuano mingine inayokuja.

Twende kwenye lengo la kuwa na timu za vijana. Mara nyingi huwa si kutwaa makombe, bali kuzalisha vipaji vya mchezaji mmoja mmoja na kuvikuza.

Na hili limefanikiwa kwa kiasi kikubwa, kwani wachezaji wengi wa Serengeti Boys wamepata nafasi ya kuonekana na mawakala mbalimbali ambao baadhi yao wapo kwenye 'akademi' mbalimbali na wengine wanatarajiwa kuchukuliwa, hivyo lengo lingine la nchi limefanikiwa.

Tuendelee kuwapa moyo wachezaji wetu kwa sababu bado wadogo na wanakua, hivyo hawa hawa baadaye wanaweza kutupa raha Watanzania ambayo hatukuitarajia.

Cha muhimu sasa ni kuangalia tangu ngazi ya familia kuacha kununua viwanja maeneo ya wazi ya kuchezea watoto na kujenga nyumba, gesti, baa, au gereji, badala yake kuwaacha watoto wacheze ili kuzalisha vipaji kwa sababu nchi inahitaji watoto wengi wenye vipaji vya hali ya juu ili kila mwaka kuwe na wachezaji wapya chini ya miaka 17 wanaoingia wawe ni wenye uwezo wa hali ya juu.

Kumbuka hata hawa waliocheza mwaka huu, baadhi yao mwakani watakuwa na miaka 18, hivyo hawatakuwa na sifa hizo tena.

Kutwaa makombe kwa timu za vijana au kufanya vizuri hakuanzii kwa serikali, wadhamini, wafadhili au Shirikisho la Soka nchini (TFF) pekee, bali hata chini kwenye ngazi za familia.

Kumkataza mtoto kucheza soka wakati ana kipaji, kuuchukua mpira ambao watoto wanacheza na kuukatakata, kuzuia kucheza kwenye sehemu ya wazi kutokana na kukosa uwanja, kote huko ni kuikosesha nchi vijana ambao wangeipa sifa na kubeba makombe.

Kwa hapa walipofika Serengeti Boys inabidi tuwapongeze, tusiwakatishe tamaa kwa sababu bado wanajifunza.

BARUA/MJADALA

## Uvaaji huu haufai, tuupige vita

**Mhariri,**

*NINAJITOKEZA leo katika gazeti letu mahiri linalotujuza habari mbalimbali zinazohusu maisha ya jamii yetu, ambazo kimsingi zinatusaidia sana kwa ajili ya maendeleo yetu kama watu binafsi na kwa ajili ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa letu hili.*

*Nimejitokeza ili kuzungumzia dukuduku inayotokana na mmomonyoko wa maadili tunaoendelea kuushuhudia kila siku, na hasa kwa upande wa vijana wetu ambao kimsingi ndiyo wanaotegemewa kuilinda nchi yetu hii.*

*Mmomonyoko wa maadili ninaouzugumzia leo ni wa upande wa staili ya uvaaji isiyo ya kimaadili, ambayo vijana wetu wanaipenda kuitumia siku hizi.*

*Pamoja na kuwa staili ya uvaaji isiyo ya kimaadili inaangukia kwa jinsia zote, lakini kwa leo ninapenda nijikite kwa vijana wa kiume.*

*Ninasema hivyo kutokana na kumshuhudia kijana mmoja wa kiume akiwa amevaa kwa staili ambayo kwa kweli hata kuiita pengine ni 'Kata K' haiwezekani, kutokana na alivyokuwa amevaa.*

*Ilikuwa ni katika basi la daladala linalofanya safari zake kati ya Tegeta Nyuki na Makumbusho.*

*Ni kwamba kijana huyo alikuwa amevaa suruali, kiuno cha suruali kikiwa magotini, na ndani akiwa na bukta kama uvaaji wa siku hizi ulivyo kwa baadhi ya vijana wetu.*

*Si kwamba aliacha miguno kutoka kwa abiria waliokuwamo ndani ya daladala hiyo tu, bali karibu watu wote walimzomea kutokana na aina hiyo ya uvaaji wake.*

*Mbaya zaidi hakupata kiti, kwa maana alisimama karibu sehemu yote ya safari yake.*

*Kupitia kwako Mhariri, nadhani wakati sasa umefika wa kurekebisha staili ya uvaaji kwa vijana wetu isiyo ya kimaadili, kwa mamlaka za kiserikali kupitisha vifungu vya sheria ndogo ndogo zinazosimamia staili za uvaaji wa mtu akiwa kwenye kadamnasi.*

**Juliana John-**
**Dar es Salaam**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Simba anzeni kujijenga sasa kwa michuano ijayo ya Caf




**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE timu ya Simba imetolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kuchapwa mabao 4-1 dhidi ya TP Mazembe ikiwa ugenini.

Simba imetolewa kwa idadi hiyo ya mabao baada ya mechi ya kwanza kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya timu hiyo hiyo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na kuhitimisha safari yake ya ajabu kwenye michuano hiyo mikubwa barani Afrika.

Wakati Simba inaanza michuano hiyo si watu wengi walioitabiria japo kutinga tu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa, achilia mbali robo fainali.

Lengo la Simba msimu huu wa kwanza baada ya kukaa misimu mitano bila kutwaa ubingwa, kwa mujibu wa viongozi wao ni kuingia makundi na hata Kocha Mkuu wa Klabu hiyo, Patrick Aussems ndiyo malengo aliyowekewa.

Kitendo cha timu hiyo kufika robo fainali ina maana kuwa klabu, wachezaji pamoja na benchi la ufundi wamevuka malengo.

Niwapongeze viongozi, wanachama, mashabiki, pamoja na benchi la ufundi kwa kufanikiwa kufika hapo ilipofikia kwani si rekodi ya Simba peke yake bali ni rekodi ya nchi nzima ya Tanzania.

Timu ambayo mara ya mwisho kutwaa ubingwa msimu wa 2011/12, ikiwa imetimu misimu mitano sasa, kutoka moja kwa moja kuchukua ubingwa hadi robo fainali ya michuano hiyo migumu barani Afrika, inastahili pongezi.

Ni miaka 15 ilipita bila ya timu yoyote ya Tanzania kutinga hatua ya makundi.

Mara ya mwisho timu ya Tanzania kutinga hatua hiyo ilikuwa ni 2003, wakati Simba hiyo hiyo ilipofanikiwa kufanya hivyo kwa kuivua ubingwa Zamaleki nchini Misri na kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa.

Hakuna timu yoyote ya Tanzania iliyofanikiwa kufika hatua ya robo fainali kwa miaka 24, lakini Simba mwaka huu imefanikiwa kufanya hivyo na kuiweka nchi kwenye nafasi nzuri ya kuongezewa timu na Shirikisho la Soka Afrika, Caf. Mara ya mwisho Tanzania kufikisha klabu kwenye hatua ya robo fainali ilikuwa ni mwaka 1994, wakati Simba ilipofanya hivyo na kutolewa na Nkana Red Devils ya Zambia kwa jumla ya mabao 3-2, ikifungwa 3-0 nchini Zambia na kushinda 2-0 nchini Tanzania.

Kwa rekodi hizi tu inaonyesha kuwa Simba imefanya kitu kikubwa sana mwaka huu na wanachama, mashabiki hawapaswi kuhuzunika, au kumlaumu mtu yeyote na badala yake kuwapongeza viongozi, wachezaji na benchi la ufundi.

Simba iliyosajiliwa msimu huu isingeweza kabisa kutwaa ubingwa wa Afrika. Haikusajiliwa kwa ajili hiyo, bali kutinga hatua ya makundi tu.

Na ndiyo maana wengi wanaona wamejitahidi sana walipofika kutokana na aina ya wachezaji waliokuwa nao.

Kila ilipokuwa ikishinda na kupanda juu, ilikutana na timu kubwa, imara, zenye wachezaji wazoefu na uwezo wa hali ya juu kuliko wao.

Ukiangalia kwa makini utagundua kuwa Simba imetolewa kutokana na wachezaji wao kukutana na wachezaji wenye uwezo mkubwa, mbinu, ubunifu, ujanja na uzoefu kuliko wao.

Na hii ni kwa sababu klabu wanazokutana nazo hatua hiyo ya juu ni zile ambazo si tu kuingia hatua ya makundi kwao ni mchezo mdogo tu kama kuua nzi, bali pia ndizo zinazotwaa kombe lenyewe.

Hata kama Simba ingeweza kuitoa TP Mazembe, ingekutana na Bingwa Mtetezi Esperance ya Tunisia ambayo ni hatari zaidi kuliko hata TP Mazembe yenyewe.

Kwa Simba hii na aina ya baadhi ya wachezaji walionao, ilikuwa si haki kutwaa Kombe la Afrika na hata kutinga tu fainali.

Bado Simba ina baadhi ya wachezaji wa nje ya nchi na ndani, hawana viwango vya kuichezea timu hiyo inayoonekana inaanza kuelekea kuwa timu kubwa Afrika.

Ili iendelee kufanya vema mwakani, kufika ilipofika au zaidi inabidi isajili baadhi ya wachezaji wa kigeni na wa Tanzania wenye uwezo wa viwango vya hali ya juu.

Kikubwa zaidi Simba ifumue eneo lote la mabeki na kulifanyia ukarabati upya, kwani imeonekana kwa michuano hiyo bado ni dhaifu, huku timu zingine zikionekana kuwa na mabeki bora, wenye uwezo mkubwa pamoja na maumbile makubwa pembeni na katikati.

Kwa kikosi hiki na hapo ilipofika, Simba inabidi ijipongeze hata kwa kuwafanyia tafrija wachezaji.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**



# Maaskofu walia rushwa

INATOKA UK. 3

hadi katika mahakama kwa kuwa hata mawakili ambao ndio watetezi wanapokea rushwa.

"Hali hii ikiachwa iendelee basi swali la haki kwetu sisi Watanzania litakua ndoto ya ahera...kitaaluma mahakimu wa namna hii wanapaswa kufutwa kama wanataaluma ya sheria," alisema Askofu Shao.

Kuhusu suala la ajira, Askofu Shao (pichani), aliiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa makini kwa wageni wanaoingia kwa mwamvuli wa uwekezaji. Alisema sio rahisi Mtanzania akaruhusiwa kuuza mitumba au 'ice cream' kwenye miji ya nchi za nje kama Roma, China, Ujerumani au New York, lakini chini ya kivuli cha uwekezaji Tanzania kuna wageni wanauza chupa za chai barabarani au kufanya kazi za vibarua viwandani.

Alisema ni vizuri serikali ikatafakari tena kuhusu mikataba yake ya uwekezaji na ajira zake.

"Uchunguzi wa kina pia ungefanyika katika hoteli zetu za kitalii na viwandani, nachelea kusema hali ilivyo haitoi matumaini kwa wasomi wetu," alisema.

Aidha aliomba serikali kutafakari kuhusu kandarasi zinazotolewa kwa wageni hasa za ujenzi kwa madai kuwa asilimia kubwa ya kandarasi hizo ni za Wachina.

Akihubiri katika ibada ya Pasaka Kanisa Katoliki la Mtakatifu Paulo wa Msalaba, Jimbo Kuu la Dodoma, Father Alex Iyulu, alisema waumini wa Kikristo wanatakiwa kuendelea kuyaishi matendo mema hata baada ya kipindi cha Kwaresima kumalizika.

"Lazima tuyaishi mambo yote mema ambayo tulikuwa tukiyafanya



katika kipindi hichi chote cha Kwaresima na kuyaenzi matendo mema aliyoyafanya Bwana wetu Yesu Krito, ambayo yametuwezesha kutuokoa katika dhambi za muovu shetani," alisema.

***Imeandaliwa na Peter Mkwavila, Paul Mabeja, Dodoma na Rahma Suleiman, Zanzibar**

# TEC yataka mikakati madhubuti bima afya

INATOKA UK. 3

kaya zote wajiunge na mfuko wa bima ya afya.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, akizungumza kwa niaba ya serikali katika ibada hiyo, aliwataka wakazi wa Kagera kuacha tabia ya kusafirisha Kahawa kwenda nchi za jirani.

Pia aliwasihi kutowasaidia wageni kupata ardhi, bali wapatiwe hifadhi kama wageni.

Kadhalika, aliwataka wakazi hao kuendelea kuliweka taifa katika sara ili amani iliyopo iendelee, huku akiahidi serikali kutoa Sh. milioni mbili kusaidia ujenzi wa kanisa hilo.

**ATAKA RIBA NAFUU YA MIKOPO BENKI**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dk. Solomon Masangwa, ameitaka serikali na mabenki nchini kutoza kodi na riba nafuu zinazowezekanazo kulipwa na wananchi wanapokopa mikopo kwenye taasisi hizo.

Akizungumza wakati wa ibada ya Pasaka katika Kanisa Kuu la Usharika wa Mjini Kati Arusha, Askofu Masangwa, alisema ni wakati kwa serikali na mabenki kujihoji kuhusu kodi kubwa na riba wanazowatoza wananchi katika mikopo kama zinalipika kiurahisi.

Alisema kuwa ili kukuza uchumi na biashara, ni lazima serikali na mabenki kuwatoza wananchi kodi na riba nafuu wanazoweza kulipa.

Masangwa alisema kulegalega kwa uchumi Tanzania serikali inajukumu la kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji kwa wananchi wake hususan vijana wapewe kipaumbele katika uwekezaji.

"Serikali na mabenki wanatoza wananchi kodi na riba kubwa ambayo siyo rahisi na hailipiki, mikopo hiyo wanakwenda kuendeleza biashara zao, hivyo ni wakati wa taasisi hizi kujihoji kama mikopo hiyo, wanayoitoa je inalipika kiurahisi na itaweza kuendeleza biashara za wananchi," alisema Masangwa.

Alisema kuwa maswali magumu ya ugumu wa maisha, changamoto za kiuchumi na biashara kwa ujumla wananchi wanapaswa kutambua kuwa majibu ya maswali hayo wanapata kwa Mungu.

Aidha ameitaka serikali kuweka mpango mkakati kwa vijana kupewa fursa za kuajiriwa na kujiajiri wenyewe bila ya kuitegemea serikali.

**Imeandikwa na Gwamaka Alipipi (Dar) na Allan Isack, (Arusha)**

# Agizo la JPM ujenzi wa stendi kaa la moto Njombe

INATOKA UK. 5

Rais Magufuli ni kutokana na hali ya hewa kuwa ya mvua kwa muda mwingi.

Mwanzinga alisema kazi kubwa ni utoaji wa kifusi, ujenzi wa maegesho ya kukata tiketi, maeneo ya kupumzika abiria ambayo yanahitaji kumiminiwa saruji pamoja na ufungaji wa milango na mageti.

"Kazi nyingine kubwa ambayo makandarasi wanatakiwa kuikamilisha ni ujenzi wa eneo la maegesho ya magari madogo ambayo mkandarasi alikuwa anashindwa kutandika vitofali vidogo vidogo ardhini kutokana na tope linalotokana na mvua," alisema na kuongeza:

"Hata kama mkandarasi akimaliza kazi kwa muda uliowekwa na Rais, bado sisi kama halmashauri hatutaruhusu kituo hiki kitumike kwa sababu maduka yaliyopo yatakuwa hayajafunguliwa kwa sababu hatujaweka matuta licha ya kwamba tumeshawapatia wafanyabiashara vibanda."

Alisema ujenzi huo ambao unatekelezwa na Kampuni ya Hanang International, unatarajia kukamilika Julai mwaka huu.

Siku hiyo, Rais Magufuli alipobaini changamoto ya kutokamilika kwa kituo hicho kwa wakati, aliwaita watendaji wake waeleze sababu za kuchelewa ndipo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji alipoeleza kuwa ujenzi wa stendi umetekelezwa kwa awamu mbili.

Mkurugenzi huyo alimweleza Rais Magufuli kuwa, awamu ya kwanza ya ujenzi ilianza mwaka 2013 na baadaye awamu ya pili, ambapo mwaka 2017, walilazimika kumtoa mkandarasi kwa sababu alichelewesha kazi.

Alisema kwa wakati huo kazi ya ujenzi wa kituo hicho ulikuwa umefikia asilimia 70 na kuahidi kuwa hadi Juni wanatarajia utakuwa umekamilika.

"Tuliingia mkataba wa Sh. milioni 792, mkandarasi akalipwa Sh. 729 ikaingia awamu ya pili Sh. bilioni 3.4 na sasa tumetumia Sh. bilioni 3.8, amekamilisha kazi zake alizokabidhiwa," alisema mkurugenzi huyo.

Mhandisi kutoka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi naye alitoa ufafanuzi kuwa mkandarasi alijenga kwa miezi 18 ndipo waziri wa wizara hiyo, Isack Kamwelwe, alimhakikishia Rais Magufuli kuwa hadi Aprili 30, mwezi huu, stendi hiyo itakuwa imekamilika.

"Tunakubaliana na halmashauri kwa hatua walizochukua nimeridhishwa na kazi za mkandarasi alizofanya hadi tarehe 30, mwezi huu, stendi itakuwa imekamilika mheshimiwa Rais," alisema.

Baada ya maelezo hayo, Rais Magufuli aliamua kuongeza siku nyingine kumi za ziada, hivyo, ujenzi wa stendi hiyo hadi kukamilika kwake, umetakiwa kutumia siku 30.

Pia aliagiza Bodi ya Makandarasi kumchunguza Mkandarasi Masasi ambaye alipewa kazi ya kujenga stendi na baadaye kuondolewa kutokana na kazi zake kuchukua muda.

Alisema mkandarasi huyo achunguzwe kwa kutumia sheria namba 17 ya mwaka 1997 ambayo inaruhusu mkandarasi kufungwa miaka mitano.

# Serikali yashauriwa

INATOKA UK. 2

kuangamiza taifa lolote huhitaji kutumia silaha za nuclear au atomic, njia nzuri ni kuharibu mfumo wa elimu.

Anaendelea kunukuu: "Ruhusu mbumbumbu waonekane wamefaulu na wasonge mbele hadi vyuo vikuu matokeo yake yatajidhihirisha baada ya muda, mbumbumbu hao wakishahitimu kwa kupata vyeti hewa, vyeti feki wagonjwa watafia mikononi mwa madaktari na manesi, majengo yataporomoka mikononi mwa wahandisi.

"Fedha zitapotelea mikononi mwa wachumi na mafisadi, utu utapotea mikononi mwa viongozi wa dini na serikali na haki itapotea mikononi mwa mahakimu na wanasheria," mwisho wa nukuu.

Askofu Rweyongeza alisema kitendo cha kuchezea elimu ni kuchezea amani na kulichezea taifa.

"Tukichambua mfumo wa elimu, je mfumo wa elimu ni biashara au haki elimu bila wajibu, kubadilishwa kwa sera na miongozo ya elimu si ishara ya wazi kwamba Watanzania bado hatujui tunachokitaka," alisema.

Alisema kama taifa linahitaji elimu bora inayomuwezesha wanafunzi kutatua changamoto za maisha ya kila siku nje ya darasa.

"Tunasoma siyo kwa ajili ya kushinda mitihani kupata vyeti, bali kwa ajili ya maisha na mfumo wa kuwezesha haya lazima uwe imara la sivyo baada ya miaka michache Tanzania itakuwa taifa la ajabu sana," alisema.

Pia alisema vijana walioandaliwa kwa gharama kubwa kuwa rasilimali watu wajenzi wa taifa na kuhudumu katika sekta viwanda na sekta nyinginezo,watajikuta ni vibarua na watumwa katika nchi yao au wataunguza viwanda na kuzika sekta hizo.

"Tayari hili limeshatokea vipindi vilivyopita viwanda ambavyo muasisi wa taifa ambaye alivipa kipaumbele vyote vilishazikwa tunamshukuru Rais John Magufuli ameshavifufua, sijui vitaendelea baada yake au tutarejea tena huko huko, tujifunze kutokana na historia tusingoje haya yatokee tubadilike."

Aidha, Askofu Rweyongeza aliwataka Watanzania waendelee kumuombea Rais Magufuli ambaye amebeba ujasiri wa kupambana na maovu yaliyokuwa yameota mizizi katika nyanja mbalimbali za utumishi wa umma,

"Rais Magufuli hachoki kutukumbusha na hachoki kumkumbusha kila mmoja wetu kuwa msemakweli ni mpenzi wa Mungu, sijui kama mna masikio ya kusikia, yaani masikio ya moyo ili yazame moyoni mwetu, tunamshukuru kwa kuonyesha mfano wa kusema ukweli," alisema.

Pia wameomba somo la dini kupewa kipaumbele mashuleni katika mtihani wa taifa kama ilivyo kwa masomo mengine kama sayansi, fizikia, kemia, bailojia, hisabati, kompyuta.

"Bila somo la dini vijana na watoto wetu wanakosa maadili ungamanifu. Pamoja na kulelewa kiakili, watoto na vijana lazima wakomazwe, kiroho na kimaadili," alisema.

Aliongeza kuwa, "Ndiyo maana katika dhama hizi kumekuwa na mafisadi wengi, wala rushwa wasiotenda haki, wabaguzi, wasiojali wala kupenda wenzao, wategeaji na watoro kazini na ofisini na utoro huo unaanzia shuleni, uharibifu kuanzia kutoa mimba hadi kuua watu wenye ualbino na vikongwe,"

Alisema vyeti vya kuhitimu pamoja na kuwa na masomo mengine liongezwe somo la dini ndani yake ili wale watakaolishinda wasiajiriwe mahali popote iwe sekta ya umma au binafsi.

Alisema ubora wa elimu hauwezi kupimwa kwa kupunguza mada au mambo anayopaswa kufunzwa kwa mwanafunzi kama ilivyo katika mtaala wa elimu ya msingi.

"Jambo lingine tunaomba serikali kuangalia upya wanafunzi kurudia darasa kama ilivyo katika kurudia mitihani, serikali iweke mfumo wa elimu ambao utasaidia vijana kuziona fursa na kuweza kuzitumia," alisema.

"Serikali iendelee kuboresha miundombinu ya kutolea elimu ikiwa ni sambamba na kuboresha maslahi ya walimu ambao ni walezi wa taifa,"alisema.

**Imeandikwa na Romana Mallya na Elizabeth Zaya**

# Mwenyekiti atozwa faini kesi ya hongo

**Na Robert Temaliilwa,** BAGAMOYO

TAASISI ya Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani imewafikisha mahakamani Mwenyekiti wa Kitongoji cha Razaba Kata ya Makurunge, Siasa Shaban Kasanuru, wafanyabiashara wawili, Idrisa Machano na Ndaju Kivalia pamoja na mlinzi wa kampuni ya Bagamoyo Sugar, Nassoro Funga kwa kosa la kutoa hongo ya Sh. 270,000.

Washtakiwa hao wanatuhumiwa kutoa hongo hiyo kwa askari polisi kinyume cha kifungu cha 15(1) (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

Washtakiwa wanadaiwa kutoa rushwa hiyo Machi 7, mwaka huu kwa askari polisi wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa wa Pwani ili wasiwakamate wakati wakiendelea kufanya biashara haramu ya mkaa na magendo katika kitongoji hicho.

Askari hao walikuwa kwenye operesheni maalumu ya kudhibiti uhalifu katika kitongoji cha Razaba kata ya Makurunge.

Kitendo cha askari hao kudhibiti mianya ya biashara haramu ya mkaa na magendo kilipelekea wafanyabiashara haramu wakiongozwa na mwenyekiti huyo wa kitongoji, Siasa Shabani Kasanura kwenda kuwashawishi polisi kwa kuwapa hongo ili wasiwakamate na wawaruhusu waendelee na biashara hiyo haramu.

Washtakiwa hao wamefunguliwa mashtaka ya jinai Na 146 ya mwaka 2019 katika Mahakama ya Wilaya ya Bagamoyo kwa kosa la kutoa hongo hiyo.

Washtakiwa wote wanne walisomewa mashtaka na Mwanasheria wa Takukuru, Beatrice Ngogo mbele ya Hakimu Mkazi, Godfrey Tumaini wa Mahakama ya Wilaya ya Bagamoyo na kukiri kutenda kosa hilo,

Baada ya kukiri kutenda kosa hilo mahakama imewatia hatiani na kutoa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu jela kwa kila mmoja au kulipa faini ya Sh. 500,000 kwa kila mmoja na kufanikiwa kulipa faini hiyo.

Naye Naibu Mkuu wa Takukuru Wilaya ya Bagamoyo, Sadiki Nombo, aliwaasa wafanyabiashara wote kufuata sheria, taratibu na kanuni ili waweze kufanya biashara zao bila usumbufu.

Nondo amewataka wafanyabiashara kufanya biashara halali kwani biashara za magendo zitawafilisi na hawatafikia malengo yao ya kibiashara.

# Kilimo cha umwagiliaji chapigwa jeki

**Na Sabato Kasika**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imewekeana mkataba na Halmashauri ya Musoma kwa ajili ya uanzishwaji wa kilimo cha umwagiliaji kwenye bonde la Bugwema lililopo Kata ya Bugwema Musoma Vijijini.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Musoma Vijijini, Charles Magoma, amesema makubaliano hayo yalifanyika Jumanne na kushuhudiwa na viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adamu Malima.

"Katika makubaliano hayo, benki itajenga miundombinu ya umwagiliaji na kutoa nyenzo za kilimo za kisasa kwa wakulima wa bonde la Bugwema na itashughulikia masuala ya usindikaji na masoko ya mazao yatakayolimwa," alisema Magoma.

Magoma alitaja mazao ambayo yataanza kulimwa kwenye bonde hilo kuwa ni alizeti, pamba, mpunga, dengu na mahindi, ambapo amewataka wakulima wajiandae kwa ajili ya kilimo hicho.

"Kwanza utafanyika upembuzi yakinifu ili kujua gharama zote za mradi huo kisha kila kitu kitajulikana, lakini tumekubaliana kwamba katika uzalishaji na faida itakayopatikana halmashauri itapata asilimia 40, huku benki hiyo ikichukua asilimia 60," alisema.

Alisema mradi huo mkubwa uliasisiwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, mwaka 1975 hadi 1978, lakini baadaye haukuendelea tena na sasa umefufuliwa upya.

"Uanzishwaji wa mradi huo wa kilimo cha umwagiliaji upo katika mtindo wa Build, Operate and Transfer (BOT) na wanufaika kwa kwanza ni wananchi wa Musoma Vijijini," alisema.

Akifafanua zaidi, mwenyekiti huyo alisema Kata ya Bugwema ina vijijini vinne alivyovitaja kwa majina ya Muoji, Kinyang'erere, Masinono na Bugwema yenyewe.

"Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Kata ya Bugwema ilikuwa na wakazi 11,251, ambao ni wafaidika kwa kuanza wa mradi huo," alisema.

Alisema bonde la Bugwema lina zaidi ya ekari 5,000 na kwamba kabla ya mkataba huo wananchi walishirikishwa wakakubali na sasa utekelezaji umefuata ili kuhakikisha kilimo cha umwagiliaji kinaanza haraka iwezekavyo.



Mkazi wa Tandale wilayani Kinondoni, akiwa kwenye taka zilizowekwa kando ya soko la Tandale ambalo halijazolewa mwishoni mwa wiki. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# BRELA sasa yawageukia wanasheria

**Na Happy Severine,** SIMIYU

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imewataka wanasheria nchini kufanya kazi kwa kufuata sheria ili kuwaondolea usumbufu wateja wao wa kubadili taarifa za leseni pasipo kuzingatia sheria ya mamlaka hiyo.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Utawala na Fedha wa Brela, Bakari Mketo, wakati wa uelimishaji wananchi kuhusu matumizi ya mfumo mpya wa online registration system (ORS), uliofanyika mjini Bariadi wakati wa mkutano mkuu wa Chama cha Wanataaluma na Wajasiriamali Wasabato (ATAPE).

Mketu, alisema baadhi ya wanasheria wamekuwa hawafuati sheria pindi wanapotengeneza au kuhuisha mkataba wa makubaliano, aidha ya kugawana au kuhamisha gawio la kampuni dhidi ya wateja wao (wafanyabiashara) na badala yake wafanye kazi kama sheria inavyowaongoza.

"Ninachoweza kusema ni kuwa sheria/wanasheria ni taaluma ambayo bado inaheshimika, kujifunza kila siku ndio taaluma inavyotaka, sisi hatuwezi kuwafundisha kazi, lakini wamekuwa wakibadili share transfer (hisa) pasipo wateja kujua ni kosa kisheria na taratibu hizo inatakiwa zifanywe na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA)," alisema Mketu.

Elizabeth Samwel wa Kampuni ya Mlashi General Supplies, iliyoko Bariadi-Simiyu, amewaambia maofisa wa BRELA kuwa mwanasheria wake alinyofoa nyaraka za mkataba wa makubaliano za kampuni hiyo na baadaye ya kubaini hali hiyo na kutoa taarifa Brela ili kupata msaada zaidi.

"Baada ya mume wangu kugundua hali hiyo, tulipiga simu Brela ili kupata ufafanuzi, tunashukuru wamekuwa pamoja na sisi na wanaendelea kutoa elimu kwetu na kwa wateja wengine," alisema Elizabeth.

Brela inaendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara jinsi ya kusajili biashara zao kwa mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao (Online Registration System-ORS).

# Waziri aitaka CCM kuibua miradi ya kuongeza mapato kujitegemea

**Na Dege Masoli,** TANGA.

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwaimu, amewataka viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kubuni na kuibua miradi kupitia rasilimali zilizopo ili kukiongezea chama hicho mapato.

Hayo aliyasema wakati akizindua mradi wa uwekezaji wa mgahawa wa kisasa wa StarCom uliojengwandani ya uwanja wa mpira wa Mkwakwani unaomilikiwa na CCM.

Ummy aliutaja uwekezaji huo kama ubunifu kwa viongozi wa CCM Wilaya ya Tanga ambao alisema licha ya kuongeza matumizi ya uwanja huo, pia chama kitapata mapato kutokana na kodi itakayolipwa na muwekezaji huyo.

Alitoa wito kwa wawekezaji kwenda sambamba na wakati huku wakizingatia ubora wa bidhaa wanazozizalisha kuwa na viwango vinavyokubalika ili kuziwezesha kuingia kwenye soko la ushindani.

Aliwataka viongozi wa chama hicho kuanzia ngazi ya kata kutumia fursa zinazowazunguka kubuni na kuibua miradi itakayo kiwezesha kupata mapato hivyo kukifanya kiondokane na utegemezi.

Awali akizungumza kabla ya mgeni rasmi, mwekezaji wa mradi huo, Sadick Shedafa, alieleza kuwa wazo la kuanzisha mradi huo limetokana na mikakati ya kukiongezea chama mapato na kwamba yeye ni muwekezaji mkodishaji kwa chama hicho.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Tobias Mwilapwa, alihimiza suala la amani na usalama akisema kuwa ni moja ya ushawishi wa watu kuwekeza huku wananchi wakinufaika na serikali kupata kodi.



Baadhi ya wafanyakazi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili kitengo cha Idara ya Ufundi wakigonganisha glasi yenye kinywaji cha shampeni wakiwa na wenza wao wakati wa hafla yao ya kupongezwa na wafanyakazi wenzao wa idara hiyo kwa kustaafu kazi kwa mujibu wa sheria, Dar es Salaam juzi **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mamlaka Ngorongoro kubuni mbinu mpya kuvutia watalii

**Na Frank Mvungi,** MAELEZO

MAMLAKA ya Hifadhi ya Ngorongoro, imesema itaendelea kuvutia watalii wa ndani na nje ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa na kuchochea ustawi wa wananchi.

Hayo yamesemwa na Mhifadhi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dk. Fredy Manongi, wakati ambapo alieleza kuwa dhamira ya Mamlaka hiyo ni kuendelea kubuni mbinu mpya za kutangaza vivutio vilivyomo ndani ya hifadhi hiyo ambavyo havipatikani katika maeneo mengine duniani wakiwamo wanyama, makundi ya ndege na kreta.

"Serikali ilichukua hatua za makusudi wakati inaanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kulinda urithi huu wa Taifa na Dunia kwa ujumla ili uweze kunufaisha kizazi cha sasa na vizazi vijavyo," Alisisitiza Dk. Manongi.

Alifafanua kuwa kutokana vivutio vilivyopo katika hifadhi hiyo kuwa vya kipekee, hali hiyo imepelekea kuongezeka kwa watalii wanaotembelea eneo hilo kila mwaka kutoka ndani na nje ya nchi, hali inayochangia kuongeza mapato yanayotokana na utalii.

Pia Dk. Manongi alitoa wito kwa Watanzania kutumia fursa ya vivutio vilivyopo nchini kwa kuvitembelea ikiwamo Ngorongoro ili kuchangia katika kukuza utalii wa ndani na kuwezesha sekta hiyo kutoa mchango stahiki katika kukuza uchumi.

Aidha, Dk. Manongi alibainisha kuwa Mamlaka hiyo imetenga Sh. bilioni 9 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kutoka kuwa za vumbi hadi kiwango cha simenti ili kuimarisha miundombinu ndani ya hifadhi hiyo.

Hifadhi ya Ngorongoro ilianzishwa mwaka 1959 ikiwa ni moja ya maeneo yanayotambulika kama urithi wa dunia na imekuwa kivutio kikubwa kwa wageni kutoka ndani na nje ya nchi kutokana na vivutio vilivyomo wakiwamo wanyama wa aina mbalimbali na ndege wa pekee ambao hawapatikani katika maeneo mengine.

# DC aonya viongozi kushiriki harusi ndoa za utotoni

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKUU wa Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, Nyabaganga Taraba, amewaonya viongozi wa Serikali ngazi ya vijiji kupewa vitu vidogo na kubariki kufanyika ndoa za utotoni, pamoja na kwenda kushiriki kula pilau kwenye harusi hizo.

Tarana amesema kwamba atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alisema ameshapewa taarifa kuwa kuna baadhi ya viongozi kwenye ngazi hizo za vijiji, wamekuwa na tabia ya kubariki ndoa za utotoni badala ya kuzizuia kutokana na kupewa kitu kidogo, na baadae huenda tena kushiriki kwenye harusi hizo na kukaa viti vya mbele.

Taraba alibainisha hayo juzi wilayani hapa alipokuwa mgeni rasmi kwenye Tamasha la Mwanamume Jasiri la kupinga mila na desturi kandamizi, ambazo zimekuwa zikikatisha ndoto za wanafunzi kwa kupewa ujauzito na kuolewa ndoa za utotoni, lililoandaliwa na Shirika la Save the Children.

Alisema ni jambo la ajabu sana kiongozi wa Serikali kubariki ndoa za utotoni, wakati ndiye anapaswa kuwa mstari wa mbele kupinga vitendo hivyo pamoja na kuwachukulia hatua kali za kisheria wahusika, lakini wao ndiyo wamekuwa wakandamizaji wakubwa wa haki za watoto kwa tamaa ya vitu vidogo.

"Natoa tahadhari kwa viongozi wa Serikali ngazi ya vijiji ambao mmekuwa mkibariki ndoa za utotoni na kwenda kushiriki kula pilau, atakayebainika nitakula naye sahani moja, yaani mtagawana hiyo miaka 30 wewe, waoaji na waozeshaji wote mtaishia jela," alisema Taraba.

Awali akisoma risala kwa niaba ya wanaume jasiri 25 ambao wamepewa mafunzo ya kupiga vita mila na desturi kandamizi za kutokomeza mimba na ndoa utotoni wilayani humo, Clement Benard, alisema changamoto ambayo imekuwa ikiwakabili ni baadhi ya viongozi wa Serikali ya vijiji kubariki ndoa hizo.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Rehema Edson, alitaja takwimu za wanafunzi mwaka huu kuanzia Januari hadi Machi akisema ambao wamekatishwa masomo kwa sababu ya kupewa ujauzito na kutaka kuolewa ni 10, wakati mwaka jana walikuwa 59.

Kwa upande wake, Meneja wa mradi wa kutokomeza mila na desturi kandamizi kutoka Shirika la Save the Children, Marry Kyando, alisema utatekelezwa wilayani humo kwenye kata 12 kwa miaka miwili, lengo likiwa ni kutokomeza tatizo la mimba na ndoa za utotoni ili kumuokoa mtoto wa kike kielimu.

# Madini vito ya mil. 363/- yanaswa mpakani

**Na Novatus Makunga,** NAMANGA

MADINI ya vito yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 363 yamekamatwa katika mashine za kukagulia mizigo ya mpakani mwa Tanzania na Kenya, katika forodha ya Namanga kati ya Februari na Machi, mwaka huu.

Madini hayo yalikuwa yanavushwa bila kufuata utaratibu wa usafirishaji nje ya nchi, yaligunduliwa katika Kituo cha Forodha cha Pamoja (OSBP), upande wa Tanzania.

Ofisa Mfawidhi Idara ya Ukaguzi wa Madini, katika Forodha ya Namanga, Anold Francis, alisema, tukio la kwanza lilitokea Februari mwaka huu kwa madini yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 329, kugundulika ndani ya mzigo wa mmoja ya wasafiri.

Alisema madini hayo yalikuwa ya aina tisa tofauti na mtuhumiwa alipaswa kulipia kodi ya asilimia saba ya thamani ya madini hayo.

Francis alisema tukio la pili lilitokea mwanzoni mwa Machi mwaka huu, pakiti nne za madini aina ya Rhodolite yenye thamani ya Sh. milioni 34 kukamatwa yakiwa ndani ya mzigo wa msafiri aliyekuwa anaelekea nchini Kenya.

Akifafanua kuhusu matukio hayo, Francis alisema kuwa kwa utaratibu wa usafirishaji wa madini kwenda nje ya nchi taratibu zinaelekeza kwamba eneo la forodha mpakani siyo sehemu ya kupatia vibali.

"Tunachofanya mpakani ni kuhakiki taratibu za kusafirisha madini kama zimefuatwa, ikiwamo ya vibali vinavyotakiwa pamoja na kodi inayopaswa kulipiwa na unapofika mpakani lazima uwasilishe nyaraka zote na siyo kupita kwa kificho," alifafanua.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ASP), Jonathan Shana, alithibitisha kutokea kwa matukio hayo yote mawili, alisema kuwa katika tukio la kwanza madini husika yamepelekwa ofisi za idara ya madini, ili kujua ni ya aina gani pamoja na uzito wake.

Aidha, katika tukio la pili Kamanda Shana alimtaja mtuhumiwa wa tukio hilo kuwa ni Mathew Mrema (46), mfanyabiashara, mkazi wa Njiro, jijini Arusha.

Wakati huo huo, Ofisa Mwandamizi wa Uhamiaji katika forodha ya Namanga Emmanuel Kajura, alisema idadi ya wageni walioingia nchini kupitia mpaka huo, waliongezeka kutoka 118,041 huku waliotoka wakiwa 106,109 kwa mwaka 2017, wakati kwa mwaka jana 2018 walioingia walikuwa 119,180 na waliotoka 106,122.

Aidha, kwa upande wa Watanzania walioondoka kupitia mpakani hapo kwa mwaka 2017, walikuwa 96,521 na walioingia walikuwa 78,328 wakati mwaka jana wa 2018 walioondoka walikuwa 77,003 na walioingia walikuwa 63,487.

Kajura alisema baada ya kuanzishwa kwa kituo cha pamoja cha forodha OSBP hivi sasa mihuri ya kuingia na kutokea nchini inagongwa katika pasi za kusafiria, katika eneo moja na hivyo kupungua muda wa kuhudumia na kuwa kati ya dakika moja mpaka dakika tatu.

Aidha, alisema hata mapato ya Visa yameongezeka kutoka dola za Marekani 836,840, kwa mwaka 2016/2017 hadi kufikia dola za Marekani 934,770, kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Kajura alisema idadi ya wahamiaji haramu nayo imepungua kutoka 59 waliokamatwa mwaka 2017 huku 23 wakikamatwa mwaka jana, wakati mwaka huu wameshakamatwa wahamiaji haramu wanne.



Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Adam Kobelo, akizungumzia Sh. milioni 16 za elimu zilizochangwa na wananchi kwenye kikao cha Baraza la Mamlaka ya Mji huo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC Muro apania kutatua migogoro

**Na woinde Shizza,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amewahakikishia wananchi wake ataendelea kutatua changamoto zinazo wakabili ikiwamo changamoto za ardhi.

Aliyasema hayo jana wakati akimtambulisha Kamanda wa Polisi mpya wa Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alipofanya ziara ya kutembelea halmashauri hiyo. Alisema kuwa ofisi yake imeweka mkakati wa kutatua kero za wananchi wake, ofisi yake imeweka wanasheria wanne ambao watawasaidia wananchi wasiokuwa na uwezo katika kesi zao mahakamani. "Kuna baadhi ya wananchi ambao wanakesi mbalimbali na wanataka msaada wa kisheria, lakini wanashindwa kuweka wanasheria kutokana na kutokuwa na uwezo, hivyo nimeamua kuwatafutia wanasheria hawa wanne ambao nitawalipa mimi mwenyewe kwa mshahara wangu mdogo ninaopewa, ili wafanye kazi ya kutatua matatizo ya wananchi yanaohusu sheria," alisema Muro.

Akiongea na wananchi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, aliwahakikishia wananchi wa Halmashauri ya Meru wilayani Arumeru, kuondoa askari yeyote atakayekiuka taratibu na kanuni za kazi yao kwa kuchafua sifa za Jeshi la Polisi.

"Napenda kuwaahidi wananchi kuwa sitamfumbia macho askari yeyote ambaye atakiuka sheria na mwananchi yeyote ambaye utaona askari anakiuka sheria, chukua simu nipigie nimshughulikie, naahidi nitasimamia vyema na sitamfumbia macho yeyote," alisema Kamanda.

Wakati huo huo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Meru, Emmanuel Mkongo, alimhakikishia kamanda huyo kumpa ushirikiano katika kazi zake za ulinzi na usalama.

Alisema anaamini bila ushirikiano katika kazi ni ngumu kila upande kutekeleza majukumu yake, hivyo watakuwa pamoja katika kupeana ushauri na masuala yatakayohitajika kwenye ofisi yake.

## Wafundwa kuacha kulalamikia serikali

**Na Mwandishi Wetu,** MANYARA

WANANCHI wametakiwa kuacha kuilalamikia serikali na viongozi wake kuwa hawawasaidii badala yake wachukue hatua kwa kufanya bidii katika kazi zao ili wafikie malengo yao ya maendeleo.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Mhandisi Zephania Chaula, aliyasema hayo jana kwenye maadhimisho ya miaka 20 ya huduma ya mtoto Tanzania, kupitia Shirika la Compassion International Tanzania, ambayo yamefanyika Mji mdogo wa Mirerani.

Chaula alisema kulalamika bila kuchukua hatua kumepitwa na wakati, hivyo jamii ihakikishe inatimiza wajibu wake ipasavyo kuliko kuilaumu serikali.

Alisema jambo kubwa ni kufanya bidii katika shughuli halali na kumtanguliza Mungu kuliko kulalamika kuwa serikali haiwasaidii au kuwalalamikia viongozi bila sababu ya msingi.

Mwezeshaji wa Klasta ya Kikatili, Audats Kisato, alisema kazi zao wanashirikiana na makanisa mbalimbali hapa nchini kwa ajili ya kueneza amani na kusaidia wahitaji.

Kisato alisema wanashirikiana ipasavyo kufanya shughuli zao, huku wakishukuru kuwapo na amani nchini kwa kuwa bila hivyo wasingeweza kufanya kazi zao.

Akisoma risala ya maadhimisho hayo, mtoto wa Kituo cha Sakila, Aneth Palangyo, alisema shirika hilo, liliingia nchini Tanzania mwaka 1999 na sasa linafanya kazi na makanisa zaidi ya 400.

Aneth alisema Klasta ya Kikatili inajumuisha makanisa sita yenye vituo vya huduma ya mtoto Mirerani TAG, JGCT, Makiba Anglican, Kikatili FPCT, Amani I. E. C, Kikatili KKKT na Sakila I. E. C.

Alisema wamefanikiwa kuwapeleka watoto shule hadi chuo kikuu, wameanzisha miradi mbalimbali na Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro aliwapa kiwanja wakamjengea mmoja wa vijana waliomsaidia kumsomesha nyumba ya kuishi.

Alisema wana changamoto ya eneo dogo la kuanzisha shule ya msingi na sekondari, vyuo, karakana ya ufundi na miradi ya kilimo na ufugaji.

"Miundombinu ya usafiri baadhi siyo rafiki, sehemu nyingine hakuna alama ya kuruhusu watoto wavuke hali inayosababisha ajali kwa vyombo vya moto," alisema Palangyo.

Katika maadhimisho hayo, Compassion International Tanzania imewakatia bima ya afya watoto 183 wa mji mdogo wa Mirerani.





# Serikali yashauriwa kutatua kero ya maji

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

WAKATI hali ya upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro ikitishia maendeleo ya ukuaji wa uchumi wa eneo hilo, serikali imeshauriwa kufanya upembuzi yakinifu kutambua maeneo yenye shida hiyo na kuhakikisha wananchi wake wanafaidi rasilimali ya maji.

Hayo yamo katika ripoti ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la kiraia la Kinshai, Veronika Shao, ambaye shirika lake linatekeleza mradi wa ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (PETS) katika Wilaya ya Mwanga.

Lengo la mradi huo ni kuijengea uwezo jamii ili iwe na ujuzi na uelewa wa kuhakikisha kunakuwapo na utawala bora na uwajibikaji katika sekta ya maji kwa kuzingatia utendaji wa sekta ya maji katika vijiji na kata husika.

"Pale ambapo serikali inaona utekelezaji wake ni mgumu, wananchi washirikishwe katika kutatua changamoto zilizopo katika maeneo yao. Hata hivyo, kutokana na tatizo la maji kuonekana ni kubwa, kuna umuhimu wa jamii husika kufikiria jinsi ya kuvuna maji ya mvua," imeeleza ripoti hiyo

Aidha, ripoti hiyo imetaka pamoja na mambo mengine, serikali iajiri na kutawanya mafundi mchundo wa maji watakaokuwa wanashughulikia matatizo ya siku kwa siku yahusuyo sekta ya maji katika jamii.

Katika ripoti hiyo, Mkurugenzi wa Kinshai ameeleza kuna haja ya kuwapo sheria ndogo ndogo za rasilimali za maji katika maeneo yote ya wilaya hiyo ambayo italinda vyanzo vya maji.

Ripoti hiyo imesema sekta ya ya maji nchini imekuwa tegemezi kwa wafadhili wa nje ambapo asilimia 88 ya fedha iliyopo ya serikali hutolewa na wafadhili wa nje na taasisi kama GIZ, Banki ya Dunia na Umoja wa Ulaya.

Ripoti pia imeibua mambo mawili ambayo ni ushiriki mdogo wa wananchi katika masuala yahusuyo maji na kukosekana kwa taarifa za mapato na matumizi.

Mradi huo unatekelezwa na Kinshai kwa ufadhili wa Shirika la The Foundation for Civil Society.

Mhadhiri wa Kitivo cha Jamii na Maendeleo Vijijini wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Prosper Kimaro, alisema utafiti huo ulifanywa katika kata za Mgagao, Lembeni, Kileo, Jipe, Lang'ata, Shighatini, Kighare, Msangeni, Mwanga na Kirya. Idadi ya washiriki wote katika utafiti huo walikuwa 365 ambao ni wanaume na wanawake.

Awali, mtaalamu mwelekezi kuhusu dhana ya ufuatiliaji wa rasilimali za umma na mchakato wa bajeti, Gamaliel Mbalase, aliwaeleza wananchi hao kuwa ufuatiliaji huo unaongeza ushiriki wa wanajamii katika ufuatiliaji wa rasilimali fedha na mchakato wa bajeti na utekelezaji wake.

Zaidi alifafanua PETS ni chombo kinachotumika katika kufuatilia au kuchunguza jinsi rasilimali za umma zinavyotumika kutoka kwenye ngazi zote za kiserikali na kisekta.

Mhandisi wa maji wa Sektretarieti ya mkoa wa Kilimanjaro, Victor Nassari, alionya kuhusu vitendo vinavyoendelea vya uharibifu wa vyanzo vya maji na baadhi ya wananchi wa kata kadhaa kugoma kufungiwa dira za maji, wakidai maji hayo hawawezi kulipia kwa sababu ni vyanzo vya asili vilivyopo katika maeneo yao.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, akizungumza na wadau hao na kamati za maji kutoka kata 10 za wilaya hiyo, alisema serikali itapambana kwa kila namna kuhakikisha miradi ya maji inayotekelezwa hakuna matumizi mabaya ya fedha wala matumizi mabaya ya madaraka.



Sista wa kanisa Katoliki ambaye jina lake halikupatikana, akiambatana na mtoto kwenda kwenye Ibada ya Sikukuu ya Pasaka eneo la mjini Kati jijini Dodoma jana. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Bil. 476/- kuchimba visima virefu

**Na Godfrey Mushi,** HAI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, imesaini mkataba maalum na mradi wa maji wa Arusha Sustainable Urban Water and Sanitation Delivery Project, kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanafaidika na maji kwa kuchimbiwa visima virefu 18.

Akitoa taarifa hiyo kwa kamati ya ulinzi na usalama iliyokuwa ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Yohana Sintoo, alisema kupitia Mhandisi wa Maji wa Wilaya wameshaweka makubaliano na hatua zote zikikamilika itaelezwa ni jinsi gani wananchi wa Hai wanaozunguka mradi huo watakavyonufaika.

Akizungumza baada ya kukagua mradi huo, Ole Sabaya alipongeza maendeleo ya mradi huo, huku akiiomba Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Arusha (AUWSA), kuisaidia Halmashauri kupata taarifa ya utafiti uliofanywa kuonyesha ni eneo gani wanaweza kuchimba visima vya maji ili kuepuka kutumia gharama nyingine za kufanya utafiti ambao tayari ulishafanywa.

Visima 18 vitachimbwa katika kata ya Masama Rundugai katika vijiji vya Chekimaji na Ngosero, na ukitarajiwa kukamilika mwakani.

Aidha, Ole Sabaya aliitaka mamlaka hiyo kuwapa pikipiki tatu maofisa watendaji wa kata kunakotekelezwa mradi huo ili kusaidia katika suala la ulinzi wa vyanzo vya maji kwa kuwa fedha nyingi za serikali zitatumika.

Mradi huo unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 476 ambazo ni sawa na Dola milioni 210.9.

Fedha zinazogharamia mradi huo mkubwa ni mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na kiasi cha Dola za Marekani milioni 22.9 ni mchango wa serikali ya Tanzania.

Kukamilika kwa mradi huo unaojulikana kama Arusha Sustainable Urban Water and Sanitation Delivery Project ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa maji katika Jiji la Arusha.

Mradi utaongeza uzalishaji wa maji kutoka wastani wa lita milioni 40 hadi kufikia lita milioni 200 kwa siku na kutoka watumiaji wa maji 325,000 hadi kufikia 600,000.

## DC achangia gari la Polisi

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

GARI la Polisi la Wilaya ya Hai ambalo limeharibika na kukwamisha baadhi ya shughuli za ulinzi na usalama wa mali za raia, limemsababisha Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya kuingiza mkono 'mfukoni' na kutoa Sh. milioni tatu za kulifanyia matengenezo makubwa.

Ole Sabaya aliyekuwa amefuatana na wadau na viongozi wa serikali, alilazimika kutoa kiasi cha fedha kwa ajili ya kugharamia matengenezo yatakayolirejesha barabarani kutoa huduma.

"Nyie pigeni mzigo, ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, wataendelea kutatua changamoto zinazojitokeza ili kurahisisha utendaji wa jeshi hili," alisema. Pia, ameahidi kutatua changamoto ya kukosekana kwa bwalo la Polisi, ukumbi wa mikutano akisema atatafuta kutoka kwa wadau wa maendeleo kiasi cha Sh.milioni 20 kuanza ujenzi huo haraka.

"Nakabidhi fedha hizi ili ziwasaidie kutatua changamoto yenu ya gari na mtambue kwamba serikali ipo pamoja nanyi na itashirikiana na jeshi kutatua changamoto zitakazojitokeza," alieleza.

Aidha, Ole Sabaya aliwataka maafisa na askari Polisi wa kufanya kazi zao kwa weledi na kuwahudumia wananchi kwa kuzingatia sheria na taratibu za kazi yao ili kuepuka malalamiko.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Upendo Wella, aliwakumbusha kufanya kazi kwa bidii kwa kuzingatia miongozo ya kazi zao.

Pamoja na mambo mengine. Ole Sabaya alitumia hadhara hiyo kumtambulisha Brighton Mushi kuwa ndiye mdau wa maendeleo atakayeshirikiana naye kufanikisha azma ya kujenga ukumbi ambaye ni mwenyeji wa wilaya ya Hai anayefanya shughuli zake mkoani Arusha.

NIPASHE JUMATATU APRILI 22, 2019
Nipashe
Spoti



WA5 WA KUPOTEA, KUTAKATA KUREJEA KWA ZIDANE MADRID UK.16



## ISIKUPITE


Cristiano Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza kutwaa ubingwa katika ligi tatu kubwa barani Ulaya, Serie A, La Liga na Premier League. Msimu huu amekuwa nguzo muhimu kwa Juventus kutwaa taji la Ligi Kuu Italia kwa kufunga mabao 19 katika mechi 27 alizocheza hadi sasa.
# MSHIKEMSHIKE...

Cristiano Ronaldo akipata upinzani mkali kutoka kwa mabeki wa Fiorentina katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Allianz juzi na wao kushinda 2-1, kwa ushindi huo Juventus ikatwaa rasmi ubingwa huo, hiyo ikiwa ni mara ya nane mfululizo.

**HABARI UK. 30**

SOKA

# KWA NINI MEUNIER AWE MRITHI WA VALENCIA UNITED?




**MANCHESTER,** England

ANTONIO Valencia ataondoka Manchester United baada ya misimu 10 ya kukumbukwa hapo Old Trafford. Ole Gunnar Solskjaer amethibititisha kwamba raia huyo wa Ecuador hataendelea kuwa mchezaji wa United kipindi kijacho cha majira ya joto.

Hata hivyo, 'Mashetani Wekundu' hao watakuwa wamepungukiwa na beki huyo wa kulia wenye umri wa miaka 33 atakapoondoka. Nahodha huyo wa klabu hiyo alikuwa chaguo la kwanza chini ya Jose Mourinho msimu uliopita. Alianza katika mechi 31 za ligi na kufunga mabao matatu.

Kiwango cha mrithi wa Valencia, Ashley Young kimekuwa kikishutumiwa vikali katika siku za hivi karibuni na pia ameshindwa kuwa kwenye kiwango kizuri katika umri wake wa miaka 30.

**Hivyo, United kwa vyovote vile watakuwa wakitafuta beki wa kulia kama ndio kipaumbele chao. Thomas Meunier amekuwa akitajwa kama ndiye mrithi sahihi wa nafasi hiyo.**

Hapa tunaangalia kwa nini United wanatakiwa kumsajili beki huyo wa PSG kwa ajili ya kurithi mikoba ya Valencia.

**UNITED INAHITAJI WINGA MWENYE UBUNIFU**

Si siri kwamba Manchester United imekuwa kwenye wakati mgumu msimu huu kutafuta winga anayejitegemea. Juan Mata, Alexis Sanchez na Jese Lingard wote wameshindwa kutoa mchango wenye manufaa kwa United.

Kwa upande mwingine, beki wa pembeni kama Antonio Valencia na Ashley Young pia hawajawa na uwezo wa kusaidia pasi za mwisho za kutengeneza nafasi za kufunga mabao. Hivyo, washambuliaji kama Romelu Lukaku na Marcus Rashford mara kwa mara wameshindwa kupata mipira kutoka winga zote mbili.

Meunier amekuwa anajulikana kwa uwezo wake wa kuanzisha mashambulizi ya kupandisha mashambulizi kutoka winga ya kulia. Amehusika katika kutengeneza mabao 14 katika mechi 38 alizocheza kwenye mashindano yote. Hivyo, anaweza kuwa msaada mkubwa wa kugawa mipira kwa washambuliajii wa United na kuweza kuimarisha timu kwa ujumla wake.

Pia ameanza kama beki wa kulia kwa wakati wote wa msimu huu na atafiti kwenye mfumo wa Solskjaer wa kuchezesha mabeki watatu. Ukiacha uwezo wake wa kupandisha mashambulizi, Meunier pia ni mzuri zaidi wa ulinzi na atatosha kuwa mrithi halali wa Antonio Valencia kuchukua majukumu yake.

**HALI YA MEUNIER PALE PSG**

Beki wa zamani wa Barcelona, Dani Alves amekuwa akichukuliwa kama ndiye kikwazo kwa Meunier msimu huu. Hadhi ya Alves kama mmoja wa mabeki bora wa pembeni asiyeshuka kiwango, imemfanya kocha Thomas Tuchel kuwa na wakati mgumu wa kuamua nani awe chaguo lake la kwanza pale PSG.

Meunier ameaanza katika mechi 16 tu kati ya 30 za PSG kwenye Ligue 1 msimu huu kutokana na ushindani mkubwa wa namba. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, hajawa kwenye chaguo la kwanza kwa miamba hao wa Ufaransa.

Pia ameshindwa kuaminiwa na PSG baada ya yeye mwenyewe kuonyesha nia ya kutaka kuhamia United. Hivyo, uwezekano wa kuendelea kucheza kwenye viunga hivyo vya Paris kwa msimu ujao ni ngumu, kwani tayari ameonyesha ana nia ya kutaka kuondoka.

Na raia huyo wa Ubelgiji anaweza kuwagharimu Man United euro milioni 35 kama wakitaka kumsajili kipindi cha majira ya joto. Na kwa namna yoyote ile uwezekano wa yeye kuendelea kucheza hapo ni mdogo tofauti na atafaa kuwa mrithi mzuri wa Valencia.

**JE, WAJUA?**



Manchester City imeshinda mechi 25 za nyumbani katika mashindano yote msimu huu, idadi ambayo ni kubwa zaidi kuwahi kufanywa na klabu yoyote ya Ligi Kuu England kwa msimu mmoja tangu Manchester United iliposhinda mechi 26 msimu wa 2010-11.

## NJE YA UWANJA

# Emery: Rekodi? Nataka kombe

UNAI Emery ameshinda mechi nyingi kuliko kocha yeyote Arsenal katika michezo yake 50 ya kwanza, lakini hilo si kitu kwake na angependa kushinda "kitu fulani muhimu".

Emery, ambaye alirithi mikoba ya Arsene Wenger majira haya ya joto, ameshinda mechi 32 kati 50 za kwanza katika uongozi wake hapo Emirates, idadi ambayo ni tisa zaidi kuliko Wenger na nne zaidi ya George Allison, ambaye alikuwa akishikilia rekodi ya sasa ya kushinda mechi 28, ambayo aliiweka mwaka 1934.

Arsenal kwa sasa inapigania kumaliza nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu England, EPL msimu huu, na inaweza kutwaa ubingwa wa Europa League baada ya kuvutia kwa kuitoa Napoli kwa jumla ya mabao 3-0 na kutinga nusu fainali ambapo sasa itakutana na Valencia.

Ray Parlour anaamini kumaliza nafasi ya nne na kutwaa ubingwa wa Europa League kutaufanya msimu wa Arsenal kuwa wa "ajabu"

Akizungumza na Sky Sports kuhusu kuvunja rekodi ya ushindi Arsenal, Emery alisema: "Ni jambo zuri kwetu kama timu na nzuri kwangu kama kocha, lakini nataka kushinda mechi zote nitakazoweza kucheza.

"Ninataka kuwa hapa na kuwa na uwezekano wa kushinda kitu fulani muhimu na Arsenal. Nadhani tunajizatiti. Lipo mikononi mwetu kufanya kitu fulani muhimu mwishoni mwa msimu.

"Ni mwenye fahari na wachezaji wetu, fahari na klabu yangu, fahari na mashabiki wetu, fahari na hali ilivyo sasa na uwezekano katika Ligi ya Europa na Ligi Kuu."






# SIMBA, YANGA NANI MTAMU KWA MATUTA?

Straika wa Yanga, Heritier Makambo, mmoja kati ya wachezaji watatu wa timu hiyo waliokosa penalti kwenye Ligi Kuu. Wengine ni Amissi Tambwe na Ibrahim Ajibu.

**Na Adam Fungamwangwo**

TIMU ya Yanga inaongoza kwa kukosa penalti kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa. Kwa mujibu wa takwimu zetu ni kwamba Yanga imekosa penalti tatu mpaka sasa, ikiwa ni nyingi zaidi kuliko timu yoyote inayoshiriki Ligi Kuu.

**Takwimu pia zinaonyesha kuwa timu za Simba na Yanga zinaongoza kwa kupata penalti nyingi kwenye Ligi Kuu. Kila moja ikibahatika kupata penalti saba.**

Jumla ya penalti 44, zimeshatolewa mpaka sasa kwenye ligi, huku Simba na Yanga zikiwa zimepata penalti 14.

Katika kile kinachoonyesha Simba ina wapigaji wazuri wa mikwaju ya penalti, timu hiyo imefunga zote saba ilizozipata kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**PENALTI SABA ZA SIMBA WAVUNI**

Penalti saba za Simba zote zimewekwa kwenye kamba na mastraika wao tegemeo, John Bocco na Meddie Kagere. Bocco amefunga penalti nne, huku Kagere akifunga tatu.

Jumatano iliyopita, Kagere alifunga kwa mkwaju wa penalti kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga na kufikisha bao la tatu la tuta, akisaidia timu yake kupata ushindi wa mabao 2-1.

Magoli mengine ya njia hiyo kwa Kagere alifunga dhidi ya Ruvu Shooting, Simba ikishinda mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Taifa na lingine dhidi ya Mbao FC kwenye Uwanja wa Jamhuri Simba ikishinda mabao 3-0.

Simba ilitumbukiza mabao mengine kwa penalti kupitia kwa nahodha wake Bocco dhidi ya Mwadui, Simba ikishinda mabao 3-1, dhidi ya African Lyon ikishinda 3-0, na mechi dhidi ya Stand United, Simba ikitakata kwa 2-0 na pia Mbao FC, ikishinda 3-0.

**PENALTI NNE ZA YANGA WAVUNI**

Wachezaji waliofunga mikwaju hiyo mpaka sasa ni Kelvin Yondani kwenye mechi ya mzunguko kwa kwanza dhidi ya Mtibwa, Yanga ikishinda mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Taifa.

Ibrahim Ajibu yeye alifunga penalti mbili kwenye mechi tofauti, ya kwanza dhidi ya JKT Tanzania, Yanga ikishinda mabao 3-0 na nyingine dhidi ya Prisons kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya ikishinda mabao 3-1.

Amissi Tambwe alipata penalti yake kwenye mechi dhidi ya Mbao, CCM Kirumba Yanga ikishinda mabao 2-1.

**TATU ZILIZOOTA MBAWA YANGA**

Penalti tatu zilizoota mbawa kwa Yanga ni ile iliyokoswa na Ajibu kwenye mechi dhidi ya Mwadui FC, Yanga ikishinda mabao 3-1, Heritier Makambo akikosa kwenye mechi dhidi ya Alliance FC, lakini timu yake ikishinda bao 1-0 na ile ya Tambwe kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Yanga ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Ndanda FC. Hii ni idadi kubwa zaidi kwa timu kukosa kwenye ligi mpaka sasa kwani timu zilizobaki zimekosa penalti moja tu.

**AZAM, MBEYA CITY, COASTAL ZIMO**

Wakati Yanga ikikosa penalti tatu, timu zingine tatu za Azam FC, Coastal Union na Mbeya City kila moja imekosa penalti moja.

Kwa maana hiyo kwenye Ligi Kuu mpaka sasa kati ya penalti 44 zilizopatikana, sita zimeota mbawa, huku 38 zikitinga nyavuni.

Azam ilikosa penalti yake kupitia kwa Enock Atta kwenye mechi dhidi ya Singida United Uwanja wa Azam Complex japo ilishinda kwa mabao 4-0.

Eliud Ambukile ambaye kwa sasa anacheza soka la kulipwa aliikosesha Mbeya City penalti kwenye mechi dhidi ya Azam, Chamazi timu yake ikichapwa mabao 2-0, huku Nteje Juma wa Coastal akikosa kwenye mechi dhidi ya Biashara, Uwanja wa Mkwakwani, lakini timu yake ikishinda bao 1-0.

## Extra Time


ASENSIO

# WA5 WA KUPOTEA, KUTAKATA KUREJEA KWA ZIDANE MADRID

**MADRID,** Hispania

KURUDI kwa Zinedine Zidane kwa mara ya pili kama kocha wa Real Madrid ni kwa ajili ya kumaliza msimu mbaya kwa Los Blancos hao. Walitolewa kwenye nusu fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'] na wapizani wao wakubwa Barcelona, wakatolewa na Ajax kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya hatua ya 16. Na wamepitwa pointi nyingi na Barcelona kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

**Mfaransa huyo amekuwa kocha wa tatu wa Real Madrid msimu huu baada ya kufukuzwa kwa kocha wa zamani wa timu ya Taifa ya Hispania, Julen Lopetegui, na baadaye Santiago Solari.**

Kurudi kwa Zidane kwenye dimba la Bernabeu kulikuja kwa mshituko hasa ikizingatiwa kwamba alijiuzulu baada ya kuwapa taji la 13 la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kushinda mara tatu mfululizo.

Hata hivyo, kurudi kwake Bernabeu kulikaribishwa na mashabiki wa Real Madrid pamoja na wachezaji. Zidane ameiongoza Los Blancos katika mechi nne. Na kurudi tena kuna ishara kwamba sasa chini ya Zidane timu imeanza kuwa kwenye ari yake ya ushindi, baada ya kuwafunga Huesca na Eibar kwenye La Liga.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao wamenufaika na walioathirika na ujio wa mfalme huyo wa mabingwa hao.

### 5. SERGIO REGUILON



Beki huyo kijana wa Hispania alijiimarisha yeye mwenyewe kama chaguo la kwanza la beki wa kushoto hapo Bernabeu chini ya kocha wa zamani wa Real Madrid, Santiago Solari. Kuingizwa kwake kwenye kikosi cha kwanza, kulimaanisha kwamba, beki mkongwe wa kimataifa wa Brazil, Marcelo, alikuwa benchi.

Hata hivyo, kurudi kwa Zidane, Marcelo haraka akarudishwa kwenye kikosi cha kwanza kwenye mchezo wa kwanza wa Zizou kama kocha wa Real Madrid. Beki huyo wa kushoto wa Brazil alikuwa ndio chaguo pendwa la Zidane wakati wa kipindi chacke cha kwanza cha ukocha hapo Real Madrid, hivyo kurudi kwake kuna maana ya kumrudisha Marcelo kwenye kikosi cha kwanza.

Kurudi kwa Marcelo katika kikosi cha kwanza cha 'Los Blancos' kutamfanya Sergio Reguilon kuangalia sasa uwezekano wa kuondoka, kwani hataweza kupenya mbele ya beki huyo mkongwe ambaye amekuwa kwenye klabu hiyo kwa miaka 13.

### 4. THIBAUT COURTOIS



Wakati Santiago Solari alipochukua mikoba ya kuinoa Real Madrid, raia huyo wa Argentina alibainisha wazi kwamba hatawachezesha magolikipa wake kwa mzunguko wa kubadilisha kama ilivyokuwa chini ya Julen Lopetegui, na alimchagua Thibaut Courtois kuwa chaguo lake la kwanza la makipa.

Hata hivyo, kurudi kwa Zizou, mambo yanaonekana kubadilika kwa kipa huyo raia wa Ubelgiji, ambapo hajacheza katika mechi zote nne za Los Blancos chini ya Zidane tangu atue tena kwa mara ya pili. Keylor Navas amerudi kuwa chaguo la kwanza, akianza katika mechi tatu.

Hata kwenye mchezo dhidi ya timu iliyopo chini ya msimamo wa Ligi, Huesca, Zidane aliamua kumuweka benchi na kwa mshangao alimchukua mwanawe, Enzo kuanza. Hiyo ni ishara kwamba muda wa Courtois kuwa chaguo la kwanza chini ya kocha huyo sasa umefikia mwisho na ataendelea kukalia benchi la hapo Bernabeu.

### 3. KEYLOR NAVAS



Keylor Navas alipata matumaini mapya ya maisha yake hapo Real Madrid baada ya kuteuliwa tena kwa Zidane kuwa kocha wa Los Blancos hao. Mfaransa huyo haraka aliamua kurudisha kikosi chake cha kwanza na raia huyo wa Costa Rica alilipa fadhila kwa Zidane kwa kudaka vizuri mechi zote tatu alizoanzishwa.

Alicheza katika mechi tatu za kwanza za Zizou hapo Bernabeu. Navas sasa alikuwa nguzo muhimu wakati Zidane akiipa Real Madrid taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo.

Wakati Zidane alipoondoka Real Madrid, Navas alimshukuru yeye kwa kumpa nafasi hiyo. Na kurudi kwake kumeimarisha mahusiano ya Real Madrid kwenye kikosi cha kwanza.

### 2. MARCO ASENSIO

Marco Asensio aliingia kwenye kikosi cha kwanza cha Real Madrid. Aliingia kwenye kikosi cha kwanza cha Los Blancos hao wakati ambao mabao yalikuwa hayapatikani.

Na chini ya Zidane alikuwa kwenye kiwango bora pia akaitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Hispania nchini Urusi.

Hata hivyo, wakati wa zama za Santiago Solari, kijana huyo chipukizi hakuwa akipewa nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Los Blancos. Kurudi kwa Zizou imekuwa na ahueni kwake kwamba atapata nafasi zaidi ya kucheza.

Hajawa kwenye kiwango kizuri bado, lakini sasa Asensio ana uhakika wa kurudi kwenye kikosi cha kwanza chini ya Zidane.

### 1. ISCO



Tangu Zidane arudi kwa mara ya pili hapo Real Madrid, inaonekana ni furaha kubwa kwa Isco ambaye hakupewa nafasi na Santiago Solari.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Hispania hakuanza mchezo wowote chini ya kocha Solari, na pia kulikuwa na uvumi kwamba ataondoka mwishoni mwa msimu huu kwa sababu hakuwa na furaha klabuni hapo.

Hata hivyo, kurudi kwa Zidane kumefufua matumaini mapya kwa Isco kurudi kwenye kikosi cha kwanza. Isco si tu kwanza alianza kuwachezea Los Blancos hao, pia alifunga dhidi ya Celta Vigo.

Isco alifungwa kwa mara ya pili mfululizo dhidi ya Huesca, na hii ni ishara kwamba Mhispania huyo atakuwa na matarajio makubwa chini ya Zidane, na atarudi kwenye kiwango chake.

## Nukuu

"Hiyo ndiyo namna ya kuwafunga mdomo [wanaoendekeza vitendo vya kibaguzi uwanjani], si kitu kizuri lakini unakifuta kwa namna hiyo. Kwa kusikitisha watu wanatumia vitu kama hivi sasa kwa sababu inatokea mara nyingi sana. Raheem Sterling alisema siku nyingine kuwa njia pekee ya kuwafunga mdomo watu kama hawa ni kufunga mabao na kuwashinda," **beki wa kushoto wa Liverpool, Andrew Robertson akizungumzia namna mchezaji mwenza wa klabu hiyo, Mohamed Salah alivyozima wabaguzi kwa bao lake murua dhidi ya Chelsea wiki iliyopita.**



"Ndiyo, kwa nini hapana. Ninajisikia kujiamini, mbio zinaendelea. Ninajua ni vita ngumu. Ninaamini kwamba nitaendelea," **Straika wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, akitangaza vita ya kuwania Kiatu cha Dhahabu EPL dhidi ya Sergio Aguero wa Man City na Mohamed Salah wa Liverpool baada ya kufunga dhidi ya Watford, hilo likiwa ni bao lake la 18, msimu huu, moja nyuma ya wawili hao.**



"Kama nilivyosema, ni mwenye furaha kwa ushindi, tumepiga hatua kidogo [kuelekea kutwaa makombe matatu]. Tunapaswa kufikiri kuhusu La Liga na kujaribu kuwa mabingwa haraka iwezekanavyo. Tutajiandaa kwa nusu fainali kwa namna mechi inavyostahili," **Lionel Messi ikiitabiria Barca kutwaa makombe matatu msimu huu baada ya kuisaidia kuichapa Man United 3-0 kwenye mechi ya mkondo wa pili ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.**



## Michezo



# SABABU SIMBA 'KULEWA' MIWA KAGERA HIZI HAPA

Baadhi ya wachezaji wa Simba wakishangilia moja ya mabao yao msimu huu.

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara nyingine tena, Simba imepokea kipigo dhidi ya Kagera Sugar.

Mara ya mwisho zilipokutana Jumamosi ya Mei 19, mwaka jana kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Ligi Kuu ya msimu uliopita, Simba ilipokea kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar mbele ya Rais, Dk. John Magufuli, mechi ambayo ilikuwa ni mbali ya kuwa ya kufunga msimu, ilichukuliwa kuwa maalum kwa ajili ya kuwakabidhi Kombe la Ubingwa wa Tanzania Bara kwani tayari ilishakuwa bingwa. Lilikuwa bao la dakika ya 84 la Edward Christopha.

**Ilikuwa Jumamosi nyingine ya Aprili 20, mwaka huu, Simba ilipokubali kipigo cha mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.**

Yalikuwa ni mabao ya Kassim Khamisi na Ramadhani Kapera, huku Emmanuel Okwi akiipatia timu yake bao la kufutia machozi.

Ufuatao ni uchambuzi unaoonyesha makosa au udhaifu uliosababisha Simba kupoteza mechi hiyo.

**1. NYODO ZA LIGI YA MABINGWA CAF**

Tangu walipotoka kucheza mechi dhidi ya TP Mazembe na kufanikiwa kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, baadhi ya wachezaji wa Simba wanaonekana kama wameridhika.

Wanaonekana hawajitumi tena na wanajiona wanajua, wamefika na kama wamezitetemesha klabu kubwa Afrika, basi hapa nchini hakuna timu ya kuwababaisha.

Hiki ndicho kinachoonekana kwani wachezaji wa Simba tangu mechi ya kwanza dhidi ya Coastal Union wanaanza mpira taratibu kana kwamba wako kwenye mazoezi hadi waliposhtuliwa na bao la mapema. Bahati nzuri tu penalti walioyoipata iliwarudisha mchezoni, lakini vinginevyo hali ingekuwa mbaya.

Hata kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar, wachezaji wa Simba hawakuonekana kama vile wanatafuta ushindi kipindi cha kwanza, kwani hata kukaba walikuwa hawakabi na kuwapa nafasi Kagera Sugara kutawala kwa muda wote. Kipindi cha pili ndipo walipoamua kucheza mpira. Kwa bahati mbaya sana kwao, tayari walikuwa nyuma kwa mabao mawili.

**2. MABEKI KUKABA KWA MACHO**

Pamoja na kwamba kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar, Simba ilicheza kwa kiwango kibovu zaidi kuliko mechi yoyote ile msimu huu, lakini waliofanya vibaya zaidi ni mabeki.

Mabeki wote wa Simba, wa pembeni na wa kati walikuwa hawakabi. Waliwaruhusu mastraika na mawinga wa Kagera kuweka mpira miguuni na kuandaa mashambulizi, huku wao wakiangalia kwa macho.

Sifa kubwa ya beki bora ni kutomruhusu mpinzani wake kuumiliki mpira kwa uhuru na kumpa nafasi ya kuufikiria aufanye nini na kuruhusu pia asipige krosi au shuti kwa uhuru.

Mabeki hao waliongozwa na Zana Coulibaly hawakufanya majukumu yao ipasavyo na kuwaacha vijana wa Kagera Sugar wakifanya wanavyotaka, hasa kipindi cha kwanza.

**3. PENGO LA WAWA LINAONEKANA**

Wapo baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba huwa hawamuamini Paschal Wawa, lakini kwa mechi mbili za Ligi Kuu ambazo imecheza bila yeye pengo lake limeonekana dhahiri.

Tangu kwenye mechi dhidi ya Coastal Union ambapo hakuwapo, safu ya ulinzi ya Simba inaonekana kuwa na mapungufu mengi.

Wawa, anaonekana kuwa ndiye beki anayeziba mapungufu ya mabeki wengine na sasa hayupo yanaonekana dhahiri. Ikumbukwe kuwa Wawa ndiye beki aliyecheza mechi nyingi zaidi za Simba kuliko mchezaji mwingine yeyote, hivyo kukosekana kwake kumekuwa na changamoto nyingi kwenye safu ya ulinzi.

Kukosekana kwake ndiko kunasababisha Simba kufungwa mabao dakika za mwanzo kabisa, na kwa mara ya kwanza imeruhusu mabao mawili, tena kwa kipindi kimoja tu. Inaonekana huenda hata Coulibaly anaonekana kupwaya zaidi kutokana na kukosekana kwa Wawa.

**4. AINA YA MABAO NI YALE YALE**

Aina ya mabao yaliyofungwa ni yale yale ya krosi. Simba imekuwa ikifungwa mabao ya aina moja. Mabao wanayofungwa ni ya kona na krosi ambazo mabeki wa kati wa Simba wamekuwa wazito au wazembe kuruka juu kuokoa hatari.

Inashauriwa kuwa krosi zote zinazopigwa, mabeki wa kati wanatakiwa wahakikisha wanakuwa wa kwanza kucheza kabla mpinzani hajaupata, au kucheza na mwili wa mpinzani ili kutomruhusu kutoupiga mpira kwa uhuru. Haya yamekuwa mapungufu makubwa ya timu hiyo hata kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika kwani mabao mengi wameruhusu kwa njia hiyo.

**5. WACHEZAJI KUSHUKA VIWANGO**

Ndani ya kikosi cha Simba kuna baadhi ya wachezaji hawako kwenye viwango vyao vya kawaida kwa muda mrefu. Lakini pia kuna baadhi ya wachezaji leo wanacheza vizuri na kesho hawako vizuri.

Hawa ndiyo walioiua Simba kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar na pia wanaweza kuiathiri timu kwenye mechi zinazofuata.

Wachezaji Emmanuel Okwi, Jonas Mkude, Paul Bukaba, kwa muda mrefu sasa hawako kwenye viwango vyao vya kawaida na kwa kiasi kikubwa wameiathiri timu kwenye mechi hiyo ambayo pia Coulibaly hakuwa kwenye ubora wake uliozoeleka.

Wachezaji Cleotus Chama, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Zana, wamekuwa na viwango vya kupanda na kushuka kulingana na mechi na kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar hawakucheza vizuri.

**NAJUA WAJUA**



Newcastle imeshinda mechi mbili mfululizo ilizocheza ugenini dhidi ya Leicester kwenye Ligi Kuu England ikiwa ni mara ya kwanza tangu Septemba 1959 ikiwa chini ya Charlie Mitten.

SOKA



# SIRI YA AJAX KUTISHA UEFA

**AMSTERDAM,** Uholanzi

LIGI ya Mabingwa Ulaya imeingia hatua nzuri zaidi, huku ikishuhudiwa Juventus wakitupwa nje kwenye michuano hiyo na vijana wadogo, Ajax.

**Wakati huo huo, Barcelona iliichapa Manchester United kwa kuweza kupata ushindi wa jumla wa mabao 4-0, wakiwa hawajaruhusu bao kwenye mechi zote mbili.**

Ajax, hata hivyo, ni farasi wenye kasi zaidi msimu huu. Wameweka historia ya kuwatoa miamba wawili wa soka la Ulaya ndani ya miezi mitatu, Real Madrid (kwenye hatua ya mtoano ya timu 16-bora) na Juventus kwenye robo fainali. Na kwa mshangao wa wengi walionyesha kiwango cha juu mno dhidi ya miamba hao.

Baada ya kupoteza kwa Real Madrid kwenye mchezo wa kwanza katika dimba la Johan Cruyff Arena, Ajax ikiwachapa vijana hao waliokuwa chini ya Santiago Solari mabao 4-1 kwenye dimba la Bernabeu. Halafu wakalazimishwa sare kwenye mchezo wa kwanza dhidi ya Juventus, lakini mabao ya Van de Beek na Matthijs de Ligt, waliwawezesha kupata ushindi wa 2-1 Ajax wakifuzu kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wachezaji kama Frenkie de Jong, De Ligt, David Neres, Dusan Tadic, na Hakim Ziyech wapo kwenye kiwango bora zaidi msimu huu na kuna uwezekano kwamba wengine hawatabakia hapo Ajax. Kwa vyovyote klabu kubwa zitataka kuwasajili wachezaji hao ili kuiimarisha timu zao.

Lakini kabla hilo halijatokea, kitu muhimu ni kujiuliza swali moja; nini kinawafanya Ajax kuwa wazuri hivyo?

**KUSHAMBULIA KWA KASI**

Kama kuna kitu ambacho kinawabeba zaidi vijana hawa, ni uwezo wao wa kushambulia kwa kasi dimbani. Ajax walicheza kwa kiwango kizuri zaidi dhidi ya Juventus na Real Madrid, na timu zote zilishindwa kuhimili mashambulizi yao.

Bianconeri walijikuta wakishindwa kabisa kusonga mbele kwa kasi, kwani mara nyingi walilazimika kuzuia mashambulizi ya vijana hao. Juve walionekana kukosa kabisa ubunifu, wachezaji wake hawakuweza kabisa kusukumiza mashambuli mbele kwa haraka.

**KIWANGO CHA JUU**

Vijana hao wa kocha Erik ten Hag walionekana kuwa kwenye kiwango cha juu zaidi, huku kila mara wakipanda kwa kasi. Juve nao walikuwa na nafasi chache, lakini De Ligt na Blind waliwafanya Juve washindwe kabisa kutengeneza tena mashambulizi ya hatari.

Ajax walimpoteza mchezaji wao muhimu Nicolas Tagliafico kutokana na adhabu, lakini hata kwa dakika moja hawakuonekana kama walikuwa wana pengo kwenye safu ya ushambuliaji au kwenye ulinzi. Kutoka kuwa timu isiyopewa nafasi, Ajax imetengeneza ari tofauti kubwa ya ushambuliaji.

Sio tu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya vijana hao wa Ten Hag pia wanakaribia kutwaa ubingwa wao wa kwanza wa Ligi Kuu Uholanzi kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2014, wamefunga mabao 106 katika mechi 30 za Ligi na wameruhusu nyavu zao kutikiswa mara 28 tu. Kiwango chao kwenye ligi ni cha kuvutia na Ajax wanaonekana wanaweza kufika mbali.

**MAWINGA WAZURI**


Ajax wamewatengeneza mawinga wazuri wakali Neres na Ziyech, ambao wakati wowote huwa wanatengeneza pasi nzuri kwa kusukumiza mashambulizi. Wote wamekuwa na ari kubwa zaidi katika mechi zote walizoichezea Ajax kuanzia kwenye ligi hadi mashindano ya Ulaya, na wote wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu kama Arsenal, Manchester United na Real Madrid.

Ukija ndani ya dimbani, Ajax wana mipango mizuri zaidi, kitu ambacho Juventus kiliwashinda. Neres na Ziyech walionekana kuwa mwiba mkali kwa kutengeneza mashambulizi mengi kutoka winga zote mbili na kuwafanya mabeki wa pembeni wa Juve kuwa kwenye wakati mgumu. Ajax wangeweza kufunga mabao mengi zaidi kama wangetumia nafasi zao vizuri.

Safu ya kiungo ya Juventus haikuwa kwenye ubora wake, kwani mipira yao yote iliishia kwa viungo wa Ajax, De Jong na Schone ambao muda wote wao ndio walikuwa na mpira.

Hii ni mara ya kwanza kwa Ronaldo kutokuwa kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu mwaka 2010. Na kwa uhakika kabisa damu changa ya vijana wa Ajax ikiwa chini ya kocha wao, Ten Hag inatarajiwa kufanya maajabu makubwa kwenye soka la Ulaya msimu huu.

**NDANI YA UWANJA**



Phil Foden amekuwa mchezaji wa tatu kinda zaidi wa Man City kuweza kufunga katika Ligi Kuu England baada ya Micah Richards na Daniel Sturridge.

Nipashe
Spotika

KURUDI kwa Zinedine Zidane kwa mara ya pili kama kocha wa Real Madrid ni kwa ajili ya kumaliza msimu mbaya kwa Los Blancos hao. Walitolewa kwenye nusu fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'] na wapizani wao wakubwa Barcelona, wakatolewa na Ajax kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya hatua ya 16.
**Uk. 16-17**

# YOSSO WANAOWATOA DENDA BARCA, REAL




JOAO FELIX

**MADRID,** Hispania

BARCELONA na Real Madrid watakuwa bize wakati wa kipindi cha majira ya joto huku kila moja ikitaka kuimarisha timu yake na kusajili majina makubwa.

Timu zote ni za uzito wa juu kwenye dunia ya mpira wa miguu na zitajaribu kujiimarisha kwa kusajili wachezaji wenye vipaji vya ukweli ili kuweza kuendelea kutawala soka la Ulaya kwa miaka mingi inayokuja.

Wakati Barcelona wapo kwenye kiwango kizuri na wakiwa na uwezekano wa kutwaa mataji matatu msimu huu, miamba hiyo ya Catalunya itakuwa na hofu ya kutofanya makosa kama ya Real Madrid walivyofanya kwenye dirisha lililopita la usajili. Wachezaji kama Messi, Suarez, Busquets, Pique na Alba umri unazidi kuwatupa mkono na wanajua vizuri kwamba wanahitaji kusajili wachezaji wenye umri mdogo ili waweze kukaa na timu hiyo kwa muda mrefu.

Wakati huo huo, Real Madrid 'Los Blancos' wanataka kujiimarisha zaidi na Rais wao, Florentino Perez akipanga kutoa kitita kikubwa cha fedha ili kumfanya kocha wake, Zinedine Zidane aweze kusajili nyota wakali. Ingawa majina makubwa yanatarajiwa kusajiliwa, lakini wanajua umuhimu wa kusajili wachezaji vijana.

Sera ya usajili ya Madrid imebadilika kwa miaka michache iliyopita. Na sasa klabu inaangalia uwezekano wa kusajili wachezaji wenye vipaji. Huku klabu zikihitaji kusajili wachezaji wenye majina makubwa ili kuweza kuleta ushindani kwenye ligi na mashindano mengine. Hapa tunawaangalia wachezaji watatu wenye vipaji ambao klabu zote mbili, Real Madrid na Barcelona zikiwania kutaka kuwasajili kipindi cha majira ya joto.

**1. JOAO FELIX**

Huku akiwa na mabao 16 na pasi za mwisho tisa katika mashindano yote kwa Benfica, Felix ana uzoefu wa kutosha kusajiliwa na timu zote mbili. Katika umri wake wa miaka 19 anatajwa kama 'Cristiano Ronaldo mpya'.

Felix ana uwezo wa kucheza kwenye winga zote na ana kasi nzuri ya kutengeneza mashambulizi kwa timu pinzani na kuwatengenezea pasi nzuri wachezaji wenzake. Uwezo wa kuichezesha timu na kuwalisha mipira wenzake ni wa hali ya juu na amekuwa nguzo kubwa kwa Benfica ambao wameitaja thamani yake kuwa ni euro milioni 120.

Huku maskauti wa 'Blaugrana' walikuwa wamefurahishwa na 'hat-trick' aliyofunga dhidi ya Frankfurt kwenye Ligi ya Europa na Los Blancos wanakifuatilia kwa karibu kipaji cha mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno. Pamoja na miamba hao wa Hispania wakiwa wanamuwania Felix, kutakuwa na ushindani mkubwa kwenye mbio za kuwania saini yake kipindi cha majira ya joto.

**2. LUKA JOVIC**

Kwa uhakika huyu naye anatajwa kuwa kwenye kilele cha kipaji chake katika umri wake wa miaka 21. Mshambuliaji huyu wa kimataifa wa Serbia amekuwa na kiwango kisichoshuka pale katika klabu yake ya Frankfurt. Huku akiwa na mabao 25 na pasi za mwisho saba katika mashindano yote, Jovic ameonyesha kwamba sasa anaweza kucheza kwenye klabu kubwa.

Jovic kwa sasa anacheza kwa mkopo kutoka Benfica, lakini Frankfurt wanaweza kumsajili mshambuliaji huyo kwa euro milioni 12 mwishoni mwa msimu huu. Jovic ana uwezo mkubwa mbele ya goli na anaonekana atakuwa na majaliwa mazuri ya baadaye.

Huku Real Madrid wakiwa wanataka kusajili sura mpya, miamba wa Katalunya wanaangalia uwezekano wa kumfanya kuwa mrithi wa Luis Suarez.

Sio siri kwamba Barcelona na Real Madrid wanamfuatilia kwa karibu nyota huyo wa Serbia kama mmoja wa chaguo lao kwenye usajili. Jovic anaweza kuwagharimu euro milioni 70.

**3. TAKEFUSA KUBO**

Kama ripoti zilivyobainishwa ni za kuaminika, Real Madrid na Barcelona wapo kwenye vita kubwa ya kumsajili raia huyo wa Japan, Takefusa Kubo, ambaye anajulikana kwa jina la utani la 'Take'. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17, ni mzuri zaidi kwenye safu ya kiungo mshambuliaji.

Take ni mmoja katika ya chipukizi waliosajiliwa na Barcelona mwaka 2011 kwa ajili ya kucheza kwenye kikosi cha wachezaji wadogo na ndio sababu Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), likaamua kuweka sheria ya kutosajili wachezaji wenye umri chini ya miaka 18 mwaka 2015. Na matokeo yake, Barcelona ililazimika kumuachia huru.

Take kwa sasa anaichezea Klabu ya Ligi Kuu ya Japan, FC Tokyo na amepotiwa kwamba ana makubaliano ya kujiunga na miamba hao wa Catalunya kama akirudi Ulaya. Licha ya kujua kwamba kuna makubaliano ya awali ya kimkataba, Los Blancos wanaweza kuwapiku wapinzani wao na kumsajili Take.

**USILOLIJUA**

Tottenham imepoteza mechi tano mfululizo za ligi ilizocheza ugenini kwa mara ya kwanza tangu Mei 2004, ilipopoteza mechi sita chini ya kocha David Pleat.





# TFS yatahadharisha ukataji miti

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imewatahadharisha wananchi kutojihusisha na vitendo vya kukata miti ovyo ili kuepukana na athari za kimazingira zinazoweka kutokea kama vile jangwa.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Meneja Msaidizi wa TFS, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Innocent Lupembe, alipokuwa akizungumza na Nipashe.

Alisema shughuli za ukataji miti na uchomaji misitu moto zimeharibu misitu.

Alisema misitu ikitunzwa na kuhifadhiwa katika mazingira mazuri italeta manufaa katika jamii, lakini pia itakuwa urithi mzuri kwa vizazi vijavyo.

Alisema jukumu la kutunza na kuhifadhi misitu sio la TFS pekee yake bali kila mwananchi anapaswa kulinda kwa kuahikikisha hakuna shughuli zozote za uvunaji, ukataji na uchomaji misitu zinafanyika.

Aidha, alisema taarifa zitolewe kwenye mamlaka kwa yeyote atakayekata miti ovyo ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Alisema mwaka huu 2019 wana kaulimbiu isemayo 'Tanzania ya kijani inawezekana tupande miti kwa maendeleo endelevu ya viwanda kuelekea uchumi wa kati', kwa kuhakikisha wanapanda miti ambayo ni rafiki kwenye vyanzo vya maji kama vile mikuyu, miembe pori, migunga na mipori.

Aidha, alisema wanawawezesha wananchi wanaoishi kandokando ya hifadhi za misitu kupanda miti ya mbao ambayo itasaidia kuongeza kipato kwenye familia zao.

Alisema Sera ya Misitu inahimiza ushirikishwaji wa wananchi katika kutunza na kuhifadhi misitu kwa faida ya sasa na ya baadaye na kuongeza kuwa sheria namba ya 14 ya mwaka 2002 inatoa muongozo na taratibu kwa mwananchi kufuata anapohitaji kuvuna misitu.

Hata hivyo Chifu wa Jiji la Mbeya, Rocket Mwashinga, aliwaomba TFS kuwaachia wao jukumu la kulinda misitu, alisema miongoni mwa kazi wanazotakiwa kuzifanya ni pamoja na kusimamia misitu.

Alisema awali wao ndio walikuwa wanasimamia na kwamba hakukuwapo na uharibifu kama ulivyo sasa hivyo wakikabidhiwa jukumu hilo rasmi shughuli za uvamizi, ukataji na uchomaji misitu ovyo zitakwisha kwa kuwa wataweka sheria za kuwabana wananchi katika maeneo yao.



Baadhi ya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Tawi la Wazalendo, Kivule, Ilala jijini Dar es Salaam, wakishirikiana kusafisha mazingira kwenye eneo la Zahanati ya Kivule hivi karibuni, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 42 ya CCM. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# TRA yaeleza umuhimu wa kutunza risiti za manunuzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

NAIBU Kamishna wa Kodi za Ndani katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Abdul Zuberi, amewataka wafanyabiashara kutunza risiti za manunuzi na matumizi, pamoja na kuweka kumbukumbu sahihi za matumizi mengine ambayo hayana risiti ili waweze kukadiriwa kodi stahiki.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kikao kilichohusisha wafanyabiashara na watumishi wa TRA mkoani Mbeya, Zuberi alisema suala la kutunza risiti za manunuzi kwa mfanyabiashara ni jambo la muhimu kwa kuwa mfanyabiashara atapata kumbumbuku sahihi ambazo zinamsaidia wakati wa kulipa kodi.

Zuberi alisema baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wavivu kutunza risiti za manunuzi na badala yake hulalamikia TRA kuwa inawakadiria mapato wakati hawana kumbukumbu za kuthibitisha.

"Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa ikitoa elimu mara kwa mara ya mlipakodi kwa wafanyabiashara nchini, juu ya umuhimu wa kutunza risiti ili waweze kulipa kodi stahiki kulingana na biashara wanazofanya, lakini imekuwa tofauti kwa baadhi yao hawafuati utaratibu na badala yake kuitupia lawama mamlaka," alisema Zuberi.

Pia alitoa elimu ya kodi pamoja na utunzaji kumbukumbu ili wafanyabiashara waweze kunufaika na serikali iweze kupata fungu lake. Alisema ni jukumu la TRA kuhakikisha hakuna mfanyabiashara anayefunga biashara kwa sababu ya changamoto za kodi na kwamba lengo ni kuhakikisha wafanyabiashara wote nchini wanafanya biashara na kulipa kodi stahiki.

Kaimu Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, David Mongate, alisema mamlaka hiyo inaendelea kuboresha mazingira mazuri ya kufanya biashara na kwamba wanataka wafanyabiashara waione TRA ni mkombozi wao na sio adui wao.

Alisema wataendelea kuboresha miundombinu ya wafanyabiashara ikiwamo kutengeneza mazingira mazuri ya ulipaji kodi ambayo haitakuwa na masharti magumu.

Baadhi ya wafanyabiashara akiwamo Agustino Mgeni, walisema suala la uandaaji wa hesabu ni changamoto kwao na kuomba TRA kutoa elimu kuhusu umuhimu huo ili wafanyabiashara hao waanze kutumia utaratibu huo.

# Biteko asitisha uchenjuaji, uchomaji dhahabu

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ameziagiza kampuni zote za kuchenjua na kuchoma dhahabu katika wilaya za Songwe, mkoani Songwe na Chunya mkoani Mbeya, kusitisha kwa muda usiojulikana shughuli hizo, baada ya kubaini mchezo mchafu wa utoroshaji dhahabu.

Biteko alisema wachenjuaji hao wameshindwa kutimiza masharti mbalimbali yanayotoa muongozo wa shughuli za uchenjuaji madini na kwamba hatua hiyo itasaidia kukabiliana na wimbi la wizi na ukwepaji kodi.

Waziri Biteko alitoa kauli hiyo hivi karibuni akiwa mkoani Songwe katika ziara yake mbalimbali yanayofanya shughuli za uchimbaji madini na kutoridhirishwa na shughuli hizo na uchenjuaji na kuamuru kusitishwa.


Kufuatia uamuzi huo, wachimbaji wadogo wa dhahabu wilayani Songwe waliiomba serikali kuwaruhusu baadhi ya wachenjuaji na wamiliki waliotimiza masharti, kuendelea na kazi wakidai kuwa kuna kila dalili za wachimbaji wanaoendesha shughuli zao kwa mikopo ya benki kufilisiwa.

Alisema baadhi ya kampuni na watu binafsi wanaofanya shughuli hizo na madini walikopa benki hivyo kusitishwa kwa shughuli hizo kumezuia ulipaji wa madeni na badala yake kumeongeza madeni.

Simon Ndaki, alisema changamoto ya kaboni kwa sasa ni kubwa na kwamba hatua mojawapo kabla ya kutoa dhahabu, watu wanakesha kuzilinda hivyo serikali inapozuia kuendelea na zoezi la kutafuta dhahabu linawakatisha tamaa na kuhofia kupoteza mali dhahabu zao na kukosa fedha.

"Ombi letu sisi wachenjuaji dhahabu na wamiliki wa kampuni za kusafisha dhahabu ni serikali kuruhusu baadhi yetu waliokidhi matakwa ya wizara kuendelea na kazi ili kujiingizia kipato ukilinganisha na ilivyosasa na shughuli zimesimama," alisema Ndaki.

Baada ya maombi hayo, Waziri wa Madini, Biteko, alisema walitoa maagizo hayo kwa sababu ya wachimbaji kutokuwa waaminifu na kwamba baadhi yao wameanza kutuma taarifa kuonyesha hatua walizozichukua hivyo muda sio mrefu baada ya kukamilisha taratibu wataruhusiwa kuendelea na uchimbaji.





# Wasabato watakiwa kuwaombea viongozi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAUMINI wa Kanisa la Waadventista wa Sabato, wametakiwa kuwaombea viongozi wa serikali ili waweze kutimiza vyema majukumu yao kwa kuwa ni watu wanaohitaji maombi.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi wa Huduma binafsi na Shule ya Sabato kutoka Jimbo la Nyanda za Juu Kusini, Mchungaji Yeriko Kasiba, katika ibada kuu ya sabato kwenye kanisa la Kizota, jijini hapa.

Alisema waumini hao na viongozi wao ni watu maalum wenye ujumbe maalum hivyo wanatakiwa kuishi katika misingi hiyo ili waweze kuisaidia jamii ikiwamo kuwatembelea na kuwafanyia maombi viongozi wa serikali.

"Sisi ni watu maalum wenye ujumbe maalum, Waadventista tumepewa jukumu hili tunapaswa kuwa kielelezo hata viongozi wa serikali wakikuona wanatambua umuhimu wako kuwa wewe ni mtu maalum mwenye ujumbe maalum," alisema.

Alisema viongozi wa serikali wanawadhamini viongozi wa dini kwa kuwa wanapenda kuombewa ili waweze kutimiza majukumu yao vyema.

Aidha, aliwataka waumini hao kuhakikisha wanaeneza injili ipasavyo ili kuongoza roho za watu waliopotea.

"Tuamke twende kazini, Yesu wakati anaondoka tukiangalia fungu la Mathayo anasema nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani kwa kuwa watu walikuwa na hofu wanasema wataendaje, lakini Yesu aliwahakikishia kuwa amepewa mamlaka," alisema.

Alisema kuna watu wanafikiri mamlaka ni kitu kidogo.

"Mnaofanya kazi serikalini mwenye mamlaka akikwambia nimetengua uteuzi wako leo halafu kesho unaweza kwenda ukasema mimi ndo Mkuu wa wilaya?" Alihoji.

Kadhalika, alisema kanisa hilo limepewa ujumbe wa malaika watatu ili kueneza injili hivyo ni wajibu wao kusimamia msingi huo.

"Enezeni Injili bila kubagua mtu yeyote kwa kuwa neno la Mungu linasema injili ihubiriwe kwa mataifa yote, watu wote wakati fulani tunapohubiri tunaruka watu fulani hatupaswi kufanya hivyo," alisema.

# Chemba wabanwa ujenzi wa hospitali

**Na Mwandishi Wetu,** CHEMBA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameagiza uongozi wa Wilaya ya Chemba kuhakikisha ujenzi wa hospitali ya wilaya unakamilika mwezi Mei, mwaka huu.

Agizo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa hospitali hiyo.

Aliutaka uongozi huo kuacha visingizio vinavyosababisha kuchelewa kukamilika kwa ujenzi huo.

"Mkuu wa wilaya, Mkurugenzi na viongozi wote hakikishe ujenzi unakamilika ndani ya muda uliopangwa ambao ni Mei, mwaka huu, kwa kuwa tayari tumeshapewa fedha za ujenzi Sh. bilioni 1.5 tusiwe na kisingizio chochote mbona wengine wamepewa fedha hizo na wamejenga," alisema. Dk. Mahenge alisema hahitaji kusikia sababu zozote zinatakazochelewesha ujenzi huo kwa kuwa maandalizi yalitakuwa kufanyika mapema.

"Pia hakikisheni mnaongeza mafundi na mtatoa fursa za Wanachemba wengi kufanya hiyo kazi, msimuachie mtu mmoja majengo yapo mengi," alisema.

Alisema kuna halmashauri zingine zimepatiwa fedha hizo zitakapomaliza mapema itaonekana viongozi wameshindwa kutimiza wajibu wao.

Naye, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Chemba, Dk. Semistatus Mashimba, alieleza kuwa changamoto zilizosababisha baadhi ya majengo kuchelewa kuanza ujenzi ni kutokana na kusubiri maelekezo kutoka Ofisi ya Rais, Tamisemi.

"Jengo la mionzi linasubiri ramani ambayo tunapewa Tamisemi na tayari tumeshaongea na Naibu Katibu Mkuu," alisema.

Mkuu wa wilaya hiyo, Saimon Odunga, aliahidi kuzingatia maelekezo ya Mkuu huyo wa mkoa ikiwamo kuongeza mafundi ili ujenzi ufanyike kwa kasi zaidi.




Wachuuzi wa vinywaji baridi wakisubiri wateja katika mataa Msimbazi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Msimamizi msitu wa Mlali njiapanda

**Na Mwandishi Wetu,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Deogratus Ndejembi, amemwagiza Kaimu Meneja wa misitu wa wilaya hiyo kumuondoa Msimamizi wa Msitu wa Mlali, Boniface Mngaje, kutokana na kukabiliwa na tuhuma za rushwa.

Aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kufanya uchunguzi wa tuhuma hizo na pia kulichunguza Baraza la Mazingira la Kata ya Ng'umbi.

Hatua hiyo ya Ndejembi ilitokana na malalamiko ya wananchi wa vijiji vya Mbagilo na Ng'umbi, waliyoyatoa katika mikutano ya hadhara aliyoifanya wakati wa ziara yake ya kutatua kero za wananchi wa wilaya hiyo juzi.

Ndejembi alisema msimamizi wa msitu huo ameshalalamikiwa kwa kiasi kikubwa tangu Mkuu huyo anaingia kwenye wilaya hiyo.

"Tangu nimekuwa Mkuu wa wilaya hapa huyo Bon analalamikiwa tu, haiwezekani wananchi wanashindwa kufanya shughuli zao kisa yeye," alisema.

Alisema wananchi ambao wamefanya kazi zaidi ya miaka 30 na wengine wana miaka 57 wapo kwenye eneo hilo la msitu huo waachwe waendelee kulima.


"Lakini lisiongezwe shamba hata moja kuingia ndani ya msitu na nyinyi wenyewe muendelee kuwa walinzi wa msitu huu, sasa aje mtu mwingine kuwabughudhi," alionya.

Kuhusu Baraza la Mazingira, Ndejembi aliagiza Takukuru wilayani humo kufanya uchunguzi wa vitendo vya rushwa kwa Mtendaji wa Kijiji cha Mbagilo, Mussa Msindai na wajumbe wa Baraza la Mazingira, Kata ya Ng'umbi.

Awali kabla ya kufikia uamuzi huo, wananchi hao walidai kuwa msimamizi huyo amekuwa akiomba rushwa kwa wakulima ili kuwaruhusu waendelee na shughuli zao kwenye maeneo ya jirani na msitu huo licha ya kuwa si eneo la hifadhi ya msitu.

Walisema upande wa mifugo imekuwa ikipigwa faini kubwa, lakini risiti inayotolewa hailingani na fedha zilizotolewa.

Baadhi yao walilazimika kukabidhi vielelezo vya risti kwa Mkuu huyo ambazo wamekuwa wakitozwa faini bila kuandikiwa kiasi au kupewa risiti za bandia.





Askofu Augustino Shao, akitoa kipaimara kwa muumini katika Ibada ya Pasaka iliyofanyika mjini Zanzibar.
**PICHA: MARTIN LABEMBA**

# Balozi Iddi ataka maadili mema mfungo Ramadhani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuuheshimu pamoja na kuutukuza mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa kutovumilia vitendo vinavyokwenda kinyume cha maadili.

Alisema tabia ya kula ovyo hadharani wakati wa mchana pamoja na mambo mengine yanayoleta ushawishi wa kuwabughudhi waumini wanaokuwamo kwenye mfungo inapaswa kuwepukwa vinginevyo atakayeendeleza tabia hiyo atachukuliwa hatua zinazostahiki.

Balozi Iddi alitoa kauli hiyo wakati akilifungua kongamano la tatu la kuukaribisha mwezi wa Ramadhani lililoandaliwa na Jumuiya ya Zanzibar Relief and Development Foundation kwa kushirikiana na Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar lililofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Sheikh Idriss Abdulwakil Kikwajuni Mjini Zanzibar.

Aliwaomba waumini wa dini zingine kuendelea na mfumo wao uliozoeleka wa kupata chakula na vinywaji majumbani mwao kitendo kinachoashiria upendo pamoja na uvumilivu wa kuheshimiana katika masuala ya kumuabudu Mwenyezi Mungu.

Alisema Ramadhani ni mwezi wa kuchuma thawabu ukibeba neema nyingi na baraka ambapo waumini wanahitaji kupata utulivu na amani katika kutekeleza ibada zao.

Balozi Iddi alieleza falsafa ya Ramadhani iliyobeba umuhimu wa kusali sala za jamaa, sala ya tarawehe, visimamo vya usiku, kuoneana huruna na kusaidiana, kutoa sadaka na zaka ni mambo yanayopaswa kuzingatiwa sio na wanakongamano pekee bali hata kwa wananchi wote.

Aliwanasihi waumini wa dini ya kiislamu na wananchi wote waendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu mara kwa mara kwa neema alizowajalia ikiwamo amani na utulivu ili azidishe baraka kwao kama alivyowaahidi katika vitabu na miongozo yake takatifu.

Alisema bila ya neema hizo hakuna jambo lolote lingeweza kufanyika akitolea mfano uwapo wa kongamano hilo lililolokusanyisha waumini kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumzia mada muhimu inayoelezea ndoa chanzo cha utu wetu iliyowasilishwa na mwanafalsafa wa dini ya kiislamu kutoka Mombasa Kenya, Sheikh Iyzudiyn Alwi, Balozi Oddo alisema ni maudhui muhimu kwa kuzingatia wakati huu ambapo kuna ongezeko kubwa la talaka katika jamii.

Alisema bila shaka mafunzo hayo yanatoa fursa kwa jamii kujifunza juu ya maisha sahihi ya ndoa kama yanavyofundishwa kwenye kitabu kitukufu cha Quran Karim na mafundisho ya kiongozi wa dini ya Kiislamu Mtume Muhammad (SAW).

Akitoa taarifa ya kongamano hilo, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Zanzibar Relief and Development Foundation (ZARDEFO), Ali Mohamed Haji, alisema taasisi hiyo itaendelea kusimamia masuala yanayostawisha jamii nchini.

Naye Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar, Khamis Juma Mwalimu, alisema kongamano hilo ni muhimu kwa vile linatoa fursa kwa waumini na wananchi kukumbushana juu ya wajibu wao.

## Mil. 154/- kukarabati jengo la wagonjwa Mnazi Mmoja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMLA ya Sh. Milioni 154 zinatarajiwa kutumika katika kukarabati jengo kongwe la kulaza wagonjwa katika Hospital ya Rufaa ya Mnazi mmoja visiwani Zanzibar ambalo limekuwa likivuja kwa muda mrefu.

Akizungumza na waandishi wa habari, msemaji wa Hospitali hiyo, Hassan Makame alisema fedha hizo zimetolewa na washirika wa maendeleo, huku ukarabati huo unatarajiwa kuanza Jumatano na utakamilika baada ya siku 28.

Alisema katika kipindi cha ukarabati wa paa la Jengo hilo shughuli za kulaza wagonjwa zitaendelea kama kawaida licha ya kuwapo mabadiliko madogo ambayo hayataathiri ukarabati huo. Alisema miongoni mwa mabadiliko hayo ni kupunguza wagonjwa wasiokuwa na ulazima wa kulazwa katika kipindi cha ukarabati na kuwaruhusu wagonjwa ambao hali zao zinaendelea vizuri.

Aidha alisema hawatohamisha wagonjwa waliolazwa kupeleka hospital nyingine badala yake watafanya utaratibu wa kuwahamishia upande mwingine ili kuepusha madhara kwa wagonjwa.

Alisema wagonjwa watakaoathrika zaidi na ukarabati wa jengo hilo ni wodi tatu ambazo mara nyingi zinakuwa na wagonjwa wengi ambazo ni ya kinamama, wagonjwa mchanganyiko na ya magonjwa ya kawaida. Alisema katika wodi ya upasuaji watapunguza operesheni isiyokuwa ya alazima ili kupunguza usumbufu.

"Tumeshauriana na wenzetu wa mamlaka ya Mji Mkongwe ambao wao wamekuja kuchunguza ni ukarabati wa aina gani ufanyike katika jengo hili, kwa hiyo hautabomoa paa lote bali tutakarabati maeneo ambayo yanavuja kwa kuweka baadhi ya mbao kama kutahitajika, maana tukilimoboa lote kama tunavyojua baadhi ya miti haipatikani tena na hata kama ipo kuipata kwake ni gharama na itachukua muda mrefu," alisema.

## Wasomi Z'bar wakosolewa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR imebahatika kukaliwa na magwiji wa fani tofauti ikiwamo, uchumi, siasa na utamaduni, lakini kwa bahati mbaya wasomi wengi wamekuwa wavivu kutafiti maisha yao na hatimae kuyawasilisha kwa jamii kwa njia ya kuandika vitabu.

Hayo yameelezwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, wakati akizindua tamthilia ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad iliyotungwa na mwandishi mahiri na mpenzi mkubwa wa lugha ya Kiswahili nchini, Prof. Emmanuel Mbogo.

Balozi Iddi alisema wakati umefika kwa wasomi au watu wa kawaida wenye uwezo na taaluma ya kuandika, kuibua na kuiweka hadharani hazina ya mashujaa wa fani mbalimbali ili vizazi vya sasa na vijavyo viweze kufaidika na michango yao.

Alisema kunakili hadhithi na kuzichapisha kwenye vitabu ni njia muafaka ya kuwaenzi mashujaa hao na itapendeza zaidi iwapo simulizi zao zitachapishwa kwa kutumia lugha mama na sanifu iliyozoeleka ya Kiswahili ili zipate wasomaji wengi zaidi.

Balozi Iddi alisema anaamini historia ya Zanzibar haiwezi kukamilika bila ya kuelezea maisha ya msanii maarufu wa taarabu Afrika Mashariki Bibi Siti Binti Saad ambapo kwa bahati nzuri Prof. Emmanuel Mbogo ameifanya kazi hiyo ya kuinawirisha historia ya Zanzibar.

Alisisitiza kwamba uandishi wa historia za mashujaa wa fani mbali mbali Visiwani Zanzibar na mwambao wa Afrika Mashariki ni muhimu kwa jamii kwa vile hadithi zao husaidia kuchangamsha na kuhamasisha kuiga mwenendo wa maisha yao. Alimpongeza na kumshukuru Prof. Mbogo kwa mchango wake wa kupanda mbegu ya mashujaa wa baadae kupitia tamthilia yake inayohusu maisha ya Siti Binti Saad inayoweza kuzalisha katika jamii.

Balozi Iddi alitoa wito kwa vijana wa sasa kuisoma tamthilia hiyo ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad na kuizingatia kwa vile inatoa funzo la umuhimu wa kung'ang'ania ndoto mpaka itowe matunda anayoyakusudia mtu.

Alisema vijana wengi wamejenga hulka ya kutojiamini na kuacha ndoto zao za kimaisha na badala yake hutafuta njia za mkato ambazo mara nyingi haziwezi kuwaletea hatma njema ya maisha yao.

Akitoa maelezo ya siku ya urithi wa utamaduni duniani Mshika Fedha wa Taasisi ya Mwanaharakati Bibi Siti Binti Saad, Aziza Saleh, alisema taasisi hiyo kupitia azimio linaloshajiisha nchi zilizomo katika uhifadhi wa urithi wa kimataifa limeandaa mambo yanayorithisha vijana kurithi tamaduni za taifa.

Naye Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Nasra Hilal, alisema yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana tokea kuasisiwa kwa taasisi hiyo miaka mitano iliyopita.

HABARI KIMATAIFA

## Ukraine yafanya duru ya pili uchaguzi wa Rais

**KIEV,** Ukraine

RAIA nchini Ukraine, jana walimiminika vituoni kwa ajili ya kupiga kura katika duru ya pili ya uchaguzi ambapo mchekeshaji kwenye vipindi vya televisheni, Volodymyr Zelensky anatazamiwa kushinda.

Uchunguzi wa maoni ulikuwa unaonesha kuwa Zelensky mwenye umri wa miaka 41 angelimshinda Rais wa sasa, Petro Poroshenko, huku kukiwa na hasira za wapigakura dhidi ya umasikini na ufisadi.

Vituo vya kura vilifunguliwa saa 11 alfajiri na kufungwa saa 11 jioni, na matokeo ya awali yalitarajiwa kutangazwa muda wowote.

Ushindi wa Zelensky ulitazamiwa kufunguwa ukurasa mpya wa historia ya nchi hiyo ambayo imekumbwa na mapinduzi ya umma mara mbili ndani ya miongo miwili na inakabiliwa na vita vya waasi wanaotaka kujitenga tangu mwaka 2014.

Ukraine inategemea misaada ya kimataifa na nishati kutoka Urusi, na rais ajaye wa taifa hilo atapaswa kukabiliana na Rais Vladimir Putin wa Urusi na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Poroshenko mwenye umri wa miaka 53 alijenga hoja kwamba Zelensky ni mpya kwenye siasa na hafai kuwa Amiri Jeshi Mkuu wakati wa vita.

Lakini muigizaji huyo wa vichekesho aliwekeza hoja zake kwa kuwaunga mkono Wananchi ambao wengi wamekuwa na hasira kwa kuchoshwa na vitendo vya rushwa, umasikini na vita ambavyo vimeshauwa takribani watu 13,000. **DW**

## Matokeo kura ya maoni Misri wiki ijayo

**CAIRO,** Misri

MAAFISA wa uchaguzi Misri wameahidi kutangaza matokeo ya kura ya maoni ya mabadiliko ya katiba Aprili 27 na kusema iwapo kadhia hiyo itapitishwa, watafanya marekebisho ya katiba mara moja.

Wananchi wa Misri walipiga kura jana kutoa maoni yao juu ya kufanyika mabadiliko ya katiba yatakayomruhusu Rais Abdel-Fatah el-Sissi kubakia madarakani hadi mwaka 2030.

Wachambuzi wa kisiasa wanasema kuwa kura hiyo ya maoni imeitishwa wakati wakosoaji wa Rais El -Sissi wakiandamwa na nguvu ya dola.

Serikali ya Misri inaendelea kuwazuia jela maelfu ya watu, wengi wao wakidaiwa ni wafuasi wa itikadi kali ingawa wachambuzi wanaeleza kuwa kuna wanaharakati wa kawaida pia kati ya hao walioko jela.

Wanaounga mkono kura hiyo ya maoni wamepongeza hatua hiyo kama ni jukumu la kitaifa, lakini wakosoaji wanalaumu kuwa ni hatua ya kuhodhi madaraka yote nchini ambako ushiriki wa kisiasa kwa wote umedidimizwa. **VOA**

# Milipuko yaitikisa Sri Lanka, 160 wafariki

**COLOMBO,** Sri Lanka

WAKATI jana dunia ikisherehekea sikukuu ya Pasaka, watu wapatao 160 wameuawa kutokana na mfululizo wa mabomu kwenye makanisa matatu na hoteli kwenye mji mkuu wa Sri Lanka, Colombo.

Milipuko sita imeripotiwa kutokea katika mashambulio dhidi ya makanisa matatu mjini Kochchikade, Negombo na Batticaloa ambayo yalishambuliwa wakati wa ibada ya Pasaka ikiendelea.

Hoteli za The Shangri La, Cinnamon Grand na Kingsbury ambazo zipo mjini Colombo, pia zililengwa katika mashambulia hayo.

**Hoteli za The Shangri La, Cinnamon Grand na Kingsbury ambazo zipo mjini Colombo, pia zililengwa katika mashambulia hayo.**

Jeshi la Polisi nchini humo limethibitisha kuwa watu wengine zaidi ya 300 wamejeruhiwa kutokana na milipuko hiyo.

Taarifa zinaeleza kuwa, Kanisa la St. Sebastian mjini Negombo limeharibiwa vibaya na milipuko hiyo. Picha zinazosambazwa katika mitandao ya kijamii zilionesha kuwa paa la jengo la kanisa lililoharibiwa vibaya huku damu ikiwa imetapakaa ndani ya kanisa, watu 67 wameripotiwa kufariki ndani ya kanisa hilo.

Pia kumeripotiwa idadi kubwa ya watu waliojeruhiwa katika kanisa la St Anthony mjini Kochchikade, ambao ni moja ya wilaya ya Colombo.

Raia tisa wa mataifa ya kigeni ni miongoni mwa watu waliouawa katika shambulio hilo.

Kwa mujibu wa msemaji wa polisi, Ruwan Gunasekera mlipuko mwingine ulitokea muda mfupi katika hoteli iliyopo jimbo la kusini mwa Colombo la Dehiwala likiwa ni shambulio la saba kufanyika katika siku ya jana, mlipuko wa nane ulitokea kwenye kitongoji cha Orugodawatta kaskazini mwa mji mkuu wa nchi hiyo.

Hadi kufikia jana hakukuwa na mtu yeyote aliyedai kuhusika na mashambulio hayo na wala idara za usalama hazijasema iwapo mashambulio hayo yalifanywa na magaidi. Lakini kumekuwa na hofu huenda wapiganaji wa kundi la Islamic State waliorejea kutoka mashariki ya kati wakawa tishio kwa usalama wa nchi hiyo.

Lakini kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari mashambulio hayo yalizilenga sehemu za kidini na kiuchumi.

Rais wa Sri Lanka, Maithripala Sirisena alisema majeshi ya ulinzi na polisi wameanzisha uchunguzi, huku viongozi mbalimbali duniani wakilaani mashambulio hayo. **DW**



Polisi na wanajeshi nchini Sri Lanka wakiweka ulinzi kwenye moja ya kanisa lililoshambuliwa. **PICHA: REUTERS**

# Marekani yamuunga mkono Haftar

**TRIPOLI,** Libya

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amemuahidi kumuunga mkono mbabe wa kivita wa Libya, Jenerali Khalifa Haftar, licha ya jitihada za Umoja wa Mataifa (UN) kusitisha mapigano ya kuwania udhibiti wa Tripoli.

Inadaiwa kuwa Rais Trump na Jenerali Khalifa walizungumza kwa njia ya simu.

Katika mazungumzo hayo, Rais Trump na Haftar walijadiliana hatua za kupambana na ugaidi na haja ya kufikia amani na utangamano nchini Libya, kwa mujibu wa Ikulu ya Marekani.

Taarifa ya Ikulu hiyo lieleza kuwa Rais Trump alilitambua jukumu muhimu la Jenerali Haftar katika kupambana na ugaidi na kulinda rasilimali ya mafuta ya Libya.

Marekani inaungana na Misri, Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu katika kumuunga mkono mbabe huyo wa kivita, ambaye mapambano yake ya kutwaa madaraka yanatishia kuirejesha tena Libya kwenye mapigano ya wenyewe kwa wenyewe.

Ikulu ya Marekani haikusema kwa nini ilichelewa kutoa taarifa ya mazungumzo hayo ya simu, lakini wachunguzi wanasema uamuzi wa Rais Trump kumsifia Haftar ni ushahidi wa kwa nini jenerali huyo amekuwa na dhamira ya kuutwaa mji mkuu, Tripoli, unaodhibitiwa na serikali inayoongozwa na Waziri, Fayez al-Sarraj, anayetambuliwa na UN.

Kamanda huyo wa kijeshi anaunga mkono serikali ya Libya yenye makazi yake mashariki mwa nchi hiyo na amekataa kuyatambua mamlaka ya serikali iliyo mjini Tripoli.

Siku ya Alhamisi, Urusi na Marekani zilipinga rasimu ya azimio la Uingereza ambalo lilikuwa likiungwa mkono na Ufaransa na Ujerumani kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kutaka usitishwaji mapigano nchini Libya.

Urusi ilisisitiza kutokuwapo ukosoaji wowote dhidi ya Haftar kwenye rasimu ya azimio hilo, huku Marekani ikitaka ipewe muda zaidi kufikiria hali ilivyo.

Licha ya kurejeshwa nyuma kijeshi, Haftar anasema kwamba anaweza kushinda, kwa mujibu wa wanadiplomasia. **DW**

# HABARI PICHA



Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Dar es Salaam, Jackson Sosthenes, akitoa baraka kwa waumini waliohudhuria ibada ya Pasaka jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Dodoma, Dk. Dickson Chilongani, akihubiria waumini jana kwenye ibada ya Pasaka katika Kanisa Kuu la Roho Mtakatifu jijini Dodoma. **PICHA PETER MKWAVILA**



Askofu Mstaafu Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Peter Mwamasika, akisalimiana na mtoto Micky Emanuel nje ya Kanisa Kuu Usharika wa Dodoma Mjini jana baada ya ibadaya Pasaka.



Baadhi ya wanakwaya ya kinamama wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Azania Front jijini Dar es Salaam, wakiimba wakati wa ibada ya Pasaka. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Wanakwaya wa Kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph, wakisikiliza mahubiri ya Askofu wa jimbo la Zanzibar, Mhashamu Augustino Shao, kwenye ibada ya mkesha wa Pasaka jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


***Kwa Habari Motomoto***

***usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Usimamiz iwa Mirathi No. 27/2019.**

Ombi la **ANASTASIUS CASSIAN PESSA** kuteuliwa Msimamizi wa Mirath iMarehemu **AURELIA R. MATAGI WA KISASA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**
**TANZANIA BARA NA VISIWANI**
**DODOMA**

Watu wotewanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 30/4/2019 kabla huyo mwombaj ihajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathihiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakama ni waweza kukaguliwa Tahehe18/4/2019

215189001

**KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ**

**Daniel Y Recco** Natangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye usajili no **T665 CGS**.

Atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu nae

Taarifa ya polisi imetolewa tarehe 18/2/2019 na kupewa no **BMG/RB/937/2019.**

215188802


**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz

au piga simu: 0767 22 33 11

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767 22 33 11

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# SIMEONE AAHIDI KUFIA UWANJANI

**MADRID,** Hispania

ATLETICO Madrid iliachwa ikipata ushindi wa 'jioni' juzi Jumamosi wakati bao la dakika ya 85 la mshambuliaji aliyetokea benchi, Thomas Lemar likitosha kuwamaliza Eibar.

Ushindi huo ulikifanya kikosi hicho cha Diego Simeone kupaa kwa pointi saba dhidi ya Real Madrid ambao walikuwa wanashuka dimbani jana Jumapili.

Na kocha huyo raia wa Argentina alisema walilazimika kupigana hadi mwisho ili kuhakikisha wanapata ushindi huo muhimu.

"Tutaendelea kupigana hadi mwisho katika kila mchezo uliopo mbele yetu ili kuhakikisha kwamba tunapata pointi zote tatu," alisema Simeone wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Katika kipindi cha kwanza nilidhani kwamba tungeweza kupata bao la mapema, lakini wapinzani wetu walikuwa na kazi na kuufanya mchezo kuwa mgumu zaidi kwetu."

Aliongeza kusema, "sasa kila mchezo uliopo mbele yetu tutacheza kwa bidii na kuhakikisha kwamba tunapata ushindi kwenye kila mchezo."

# Man City yapanga kumsajili Sancho

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City inapanga kuingia kwenye vita na Manchester United kwenye mbio za kumsajili nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho.

Winga huyo wa England anaonekana kuwa kwenye rada za kocha Ole Gunnar Solskjaer kuelekea kwenye dirisha la uhamisho la kipindi cha majira ya joto.

Dortmund ilimsajili Sancho kutoka Uwanja wa Etihad kwa pauni milioni 10, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, amekuwa kwenye kiwango bora zaidi hapo kwenye dimba la Westfalenstadion.

Kwa mujibu wa Gazeti la Bild, City inapanga kumsajili Sancho na kumrudisha katika kikosi hicho.

Hata hivyo, taarifa kutoka kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, zinasema kwamba, hawatakuwa tayari kumuachia mchezaji huyo mwishoni mwa msimu huu.






# *Valverde amtetea Philippe Coutinho*

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde, amepuuzia mgongano uliopo kati ya kiungo wake, Philippe Coutinho na mashabiki wa klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ameshindwa kufikia matarajio ya mashabiki wa Nou Camp baada ya kujiunga akitokea Liverpool kwa pauni milioni 142 Januari mwaka 2018.

Huku taarifa zikisema kwamba, mchezaji huyo ataondoka kipindi cha majira ya joto mwaka huu.

Mashabiki wa Blaugrana hao walimzomea Coutinho wakati alipoingia kwenye mchezo wa ushindi wa 2-1 wa Jumamosi dhidi ya Real Sociedad.

Zomea ya mashabiki hao imekuja baada ya mchezaji huyo kufunga bao kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester United na kuonyesha ishara ya kuziba masikio kwa vidole na kufumba macho.

Hata hivyo, Valverde amekanusha Coutinho kutokuwa na uhusiano mazuri na mashabiki wa Barcelona.

Baada ya mchezo huo dhidi ya Sociedad aliulizwa kuhusu uhusiano wa Coutinho na mashabiki wa klabu hiyo akisema kuwa hakuna kitu kibaya kinachoendelea.

## HABARI MICHEZO



# AMIR KHAN ACHEZEA KICHAPO MAREKANI

**NEW YORK,** Marekani

BONDIA wa Uingereza, Amir Khan, usiku wa kuamkia jana amejikuta akikumbana na kipigo kikali kutoka kwa mpinzani wake, Terence Crawford wa Marekani.

Kwenye pambano hilo la ubingwa ambalo limepigwa alfajiri ya kuamkia jana katika Ukumbi wa Madison Square Garden jijini New York Marekani, Crawford alionekana kutawala kwa muda wote hadi raundi ya sita alipomaliza pambano kwa kumtwanga TKO Amir.

Baada ya kipigo hicho, Amir ameomba radhi kwa mashabiki wake kwa kudai kuwa hakupenda kutoendelea na pambano, lakini alijisikia maumivu makali.

"Sikupenda kabisa kutoendelea na pambano, lakini nilizidiwa na maumivu makali, nawaomba radhi mashabiki wangu, mchezo ulikuwa unavutia na ningependa kuendelea kama mwamuzi asingesitisha pambano kwa muda mfupi," alisema Khan muda mfupi baada ya kumalizika kwa pambano hilo.

Amir amekuwa akishambuliwa na mashabiki wake kwenye mitandao ya kijamii kwa kumuita 'biskuti' hii ni kutokana na kuwa mwepesi pindi anapopigwa masubwi mazito.

# Guardiola: Muziki wa Liverpool acha kabisa

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema kwamba, wapinzani wao kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu, Liverpool ni moja ya timu bora ambayo hajawahi kuiona kwenye maisha yake.

City inaongoza msimamo wa Ligi Kuu kwa tofauti ya pointi moja dhidi ya 'Wekundu' hao baada ya kuwafunga Tottenham 1-0 juzi Jumamosi.

Timu zote zimebakiwa na mechi nne ili kumaliza ligi hiyo, huku Liverpool jana ilikuwa na nafasi ya kurudi kileleni wakati walipocheza na Cardiff City.

"Taji bado lipo mikononi mwetu," alisema Guardiola. "Kila siku nikiiangalia Liverpool naiona ina wachezaji ambao wanakifanya kikosi chao kuwa bora," alisema Guardiola akinukuliwa na Sky Sports.

"Tutaona wapi tutafika. Tunapigana na timu bora na tutaona mwisho wa siku nani atakuwa bora, lakini wao Liverpool ni bora zaidi."



# *Man united yakosolewa kumpa ukocha Solskjaer*



**MANCHESTER,** England

MCHEZAJI wa zamani wa Timu ya Taifa ya Uingereza, Jermaine Jenas, ameponda uamuzi wa Klabu ya Manchester United kumpa ajira ya kudumu Ole Gunnar Solskjaer.

Jenas ambaye aliwahi kuchezea klabu za Newcastle United, Tottenham Hotspur, Aston Villa na Queens Park Rangers amesema anadhani klabu hiyo haikujua inachofanya wakati wa kufikia uamuzi huo ambao amedai ulitokana na kuzidiwa hisia kwa mafanikio ya awali ya Solskjaer.

Solskjaer aliibeba Manchester United katika kipindi cha mpito akichukua nafasi ya aliyekuwa kocha wa klabu hiyo, Jose Mourinho ambaye alifukuzwa Desemba mwaka jana baada ya kupata matokeo mabaya mfululizo.

Kocha huyo mwenye rekodi ya kushinda Kombe la Mabingwa akiichezea klabu hiyo mwaka 1999, aliingia na bahati ya aina yake akishinda michezo 10 kati ya 11, hatua iliyowavutia Manchester United na kumtunuku mkataba wa kudumu Machi mwaka huu.

Lakini hivi karibuni bundi ametua kwenye kazi ya kocha huyo, ambapo amesha-poteza michezo mitano kati ya michezo saba ikiwa ni pamoja na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona. Hali hiyo ndiyo iliyomfanya Jenas kukosoa uamuzi wa 'Mashetani Wekundu' hao wa Old Trafford.

"Mimi nadhani ulikuwa uamuzi wa kihisia zaidi, lakini kwenye biashara kunapaswa kuwa na uamuzi unaofikiria muda mrefu ujao. Alichokifanya Alex Ferguson kilikuwa cha kipekee sana na United, wamekuwa na wakati mgumu sana kumpata meneja kama yeye," Janes aliwaambia waandishi wa habari.

"Pep Guardiola alipoenda Manchester City hakusema 'Roberto Mancini na Manuel Pellegrini walifanya nini kushinda ligi? Aliingia na kufanya kile ambacho alitaka kufanya. Lakini nadhani Manchester United hawajui wanachokifanya sasa," aliongeza.

Klabu hiyo hivi sasa iko katika nafasi ya sita kwenye ligi ikiwa na alama mbili nyuma ya Arsenal na Chelsea ambao wako katika nafasi ya nne na tano.

# DONDOO ZA SO
# MAGAZETI YA U




# RONALDO ANUKA REKODI JUVE IKITWAA UBINGWA

## Mabao yake yaliiwezesha timu hiyo kupata pointi kwenye Serie A, akitengeneza pointi 16...

**TURINI,** Italia

WAKATI Cristiano Ronaldo alipokamilisha uhamisho wale wa euro milioni 112 kutoka Real Madrid kwenda Juventus Julai mwaka 2018 katika umri wa miaka 33, kuliibuka maswali mengi kama ataweza kuwa na uwezo wa kuwa na kiwango kilekile kama alichokuwa nacho Hispania.

**Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or alianza taratibu, akishindwa kufunga kwenye mwanzo wake wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, hadi Septemba wakati aipofunga mara mbili huku Juve ikiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Sassuolo.**

Halafu akaanza kufunga mara kwa mara na kuimarisha mafanikio ya 'Bianconeri' hao kutetea ubingwa huo.

Akafunga tena mara mbili dhidi ya Empoli, Sampdoria na Parma kabla ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno kufunga 'hat-trick' katika ushindi wa 3-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora dhidi ya wapinzani wake wa zamani, Atletico Madrid.

Kocha wa Juve, Massimiliano Allegri amekuwa akiwachezesha kwa zamu Douglas Costa, Mario Mandzukic na Paulo Dybala kama safu yake ya washambuliaji watatu, huku Moise Kean aliingia kwenye kikosi hicho mwishoni mwa msimu huu na kuwa patina wa Ronaldo.

Ushindi wa Juve wa 2-1 dhidi ya Fiorentina Jumamosi uliwawezesha kutwaa kwa mara ya nane mfululizo taji la Scudetto kwa Juve, na Ronaldo amekuwa na mchango mkubwa kwenye ubingwa huo na akikaribia kufikisha mabao 600 aliyofunga katika ngazi ya klabu.

Mabao ya Ronaldo yaliiwezesha timu hiyo kupata pointi kwenye Serie A, akitengeneza pointi 16 katika mabao 19 aliyofunga. Mshambuliaji huyo ni mchezaji wa kwanza kwenye historia ya Serie A kuifungia timu yake katika mechi nane mfululizo kwa msimu mmoja, akifunga mabao 10.

Ronaldo amefunga mabao mawili kwenye mchezo mmoja mara nne kwenye Serie A msimu huu, tatu kati ya hayo ni kwenye Uwanja wa Allianz. Nyota huyo wa Juve amefunga dhidi ya timu 13 tofauti kwenye Serie A.

Mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United amefunga mabao 12 katika nusu ya pili ya Serie A msimu huu. Ronaldo ndiyo mchezaji aliyepiga mashuti mara nyingi zaidi, akipiga mashuti mara 165 kuelekea golini kwenye Serie A msimu huu.

Hakuna mchezaji aliyelenga goli mara nyingi zaidi kwenye Serie A msimu huu kuliko Ronaldo, alilenga mara 65.

Kadhalika, Ronaldo sasa amekuwa mchezaji wa kwanza kuweza kutwaa ubingwa katika ligi tatu kubwa barani Ulaya, Serie A, La Liga na Premier League. Msimu huu amekuwa nguzo muhimu kwa Juventus kutwaa taji la Ligi Kuu Italia kwa mara ya nane mfululizo akifunga mabao 19 katika mechi 27 alizocheza hadi sasa.

## ZISIKUPITE

### RASHFORD KUPANDIWA DAU

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford, 21, anajiandaa kupandiwa dau ili kujiunga na Barcelona kwa sababu wanahisi itakuwa ni vigumu kumng'oa kutoka Old Trafford. ***(Express)***

### SPURS YAJIAMINI KWA ERIKSEN

TOTTENHAM imeongeza kujiamini kuwa kiungo Christian Eriksen ambaye amekuwa akihusishwa na Real Madrid, atasaini mkataba mrefu kuitumikia. ***(Goal.com)***

### ZAHA KUSHTUKIZWA KUTUA PSG

PARIS St-Germain ipo tayari kufanya usajili wa kushtukiza kwa kutoa ofa ya pauni milioni 65 kwa mshambuliaji Wilfried Zaha, 26, ambayo moyo wake u-radhi kuachana na klabu hiyo majira haya ya joto. ***(Express)***

### UTD YAMCHANGANYA DE GEA

KIPA wa Manchester United, David de Gea, ameendelea kuchanganywa kutokana na klabu hiyo kutokubali kufikia ombi lake la muda mrefu la ongezeko la malipo. ***(Times)***

### AKATAA KUMTAJA MBAPPE

KOCHA Zinedine Zidane, ambaye amekuwa akihusishwa na kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, 20, amekiri kuwa atafanya mabadiliko katika mfumo wa uchezaji wa klabu hiyo msimu ujao, akakataa kujadili anaowawinda. ***(London Evening Standard)***

### KUZIVUTA LIVER, ARSENAL

KIUNGO wa Ajax, Hakim Ziyech, 26, anapatikana sokoni kwa pauni milioni 25 tu, jambo ambalo linaziweka Man City, Manchester United, Arsenal na Liverpool katika mkao wa kumwania. ***(Mirror)***

### BALE ATOA MASHARTI KUUZWA

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Gareth Bale, 29, anaweza kuchagua kutimkia kwenye 'mahela' mengi China, Falme za Kiarabu na Ligi Kuu Marekani (MLS), pamoja na klabu kubwa Ulaya, lakini ni endapo tu atalipwa zaidi ya dau lake la sasa linaloelezwa kuwa pauni 500,000 kwa wiki, vinginevyo nyota huyo wa kimataifa wa Wales atabaki katika klabu hiyo hadi mkataba wake utakapomalizika mwaka 2022. ***(Mirror)***

### FELIX, JOVIC MTEGONI CITY

MANCHESTER City inapanga kwenda kumsajili kiungo mshambuliaji wa Benfica, Joao Felix, 19, na pia imekuwa ikimfuatilia Luka Jovic wa Frankfurt ***(Goal.com)***

### PHELAN AVUTIWA UKURUGENZI

KOCHA msaidizi wa Manchester United, Mike Phelan, hajakubali kuongezewa mkataba na inaaminika anavutiwa na nafasi ya mkurugenzi wa michezo. ***(Mirror)***

### SULE KATIKA ORODHA YA UTD

BEKI wa kati wa Bayern Munich, Niklas Sule, 23, amekuwa beki mpya kwa sasa kujumuishwa katika orodha ya wachezaji wanaohitajika na Manchester United majira haya ya joto. ***(Sport1, via Mirror)***

### YAJIULIZA KWA WAN-BISSAKA

CRYSTAL Palace inataka pauni milioni 80 kwa Wilfried Zaha, lakini haitaki kuwauza wote Muivory Coast huyo pamoja na beki wa kulia Aaron Wan-Bissaka, 21, katika majira haya ya joto. ***(Mail)***

## HABARI MICHEZO

# ZFA yapitisha katiba mpya

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUTANO Mkuu wa Chama cha Soka Zanzibar (ZFA), umepitisha katiba mpya ya chama hicho bila kupingwa ambayo sasa itaanza kutumika rasmi katika shughuli zote za soka la visiwani hapa.

Mkutano huo mkuu uliofanyika kisiwani Unguja katika Ukumbi wa Uwanja wa Amaan, ulihudhuriwa na wajumbe tisa kati ya 10 wa mikoa mitano ya Zanzibar ambao ni wenyeviti na makatibu wao kutoka Unguja na Pemba.

Katika upitishwaji wa katiba hiyo, wajumbe tisa waliokuwapo ukumbini hapo walikubali kupitisha katiba hiyo huku mjumbe mmoja kutoka mkoa Mjini Magharibi ndiye hakuhudhuria kutokana na matatizo ya kiafya.

Katiba hiyo sasa inaliondoa jina la ZFA na kuwa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), dhamira yake ni kuweza kufikia malengo ya kukuza soka la Zanzibar katika ngazi zote kuanzia chini.

Akizungumza na Waandishi wa habari mara baada ya kumalizika mkutano huo Katibu wa Chama hicho ambapo kwa sasa ZFF, Mohamed Ali, alisema mchakato unaofuata sasa ni kufanya uchaguzi mkuu wa chama hicho kupitia katiba hiyo mpya ambayo imepitishwa jana.

Alisema punde kamati ya uchaguzi itakapotangazwa na wao watakuwa na jukumu la kushugulikia taratibu hizo za uchaguzi wa rais, makamu na wajumbe wa kamati utendaji.

"Katiba hii ina mambo mengi ambayo yatapeleka soka letu mbele kuanzia nganzi ya chini kabisa, kikubwa viongozi watakaochaguliwa waifuate na wahakikishe yale ambayo yamependekezwa,"alisema.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yangas | 32 | 23 | 5 | 4 | 51 | 23 | 74 |
| 2. Azam | 32 | 19 | 9 | 4 | 49 | 19 | 66 |
| 3. Simba | 24 | 19 | 3 | 2 | 51 | 10 | 60 |
| 4. Mtibwa Sugar | 32 | 14 | 6 | 12 | 33 | 24 | 48 |
| 5. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 6. Ndanda | 32 | 11 | 10 | 11 | 22 | 30 | 43 |
| 7. Kinondoni MC | 31 | 9 | 15 | 7 | 32 | 22 | 42 |
| 8. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 9. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 10. Singida United | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 11. Kagera Sugar | 32 | 9 | 12 | 11 | 28 | 33 | 39 |
| 12. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 19 | 26 | 39 |
| 13. Stand Utd | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 14. Mbeya City | 31 | 10 | 7 | 14 | 30 | 34 | 37 |
| 15. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 16. Alliance | 32 | 9 | 10 | 13 | 23 | 33 | 37 |
| 17. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara Utd | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# MIRAMBO AOMBA RADHI VIPIGO SERENGETI BOYS

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na timu yake kufanya vibaya kwenye fainali za Mataifa ya Afrika kwa Vijana chini ya miaka 17 (Afcon U-17) ambazo zinaendelea nchini, Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Oscar Mirambo, amewaomba radhi Watanzania kwa matokeo hayo mabaya.

**Serengeti Boys ambao walikuwa wenyeji wa fainali hizo walipoteza mechi zao zote tatu za Kundi A ambalo lilijumuisha pia yosso kutoka Nigeria, Angola na Uganda.**

Waliosonga mbele na kukata tiketi ya kucheza Fainali za Dunia za Vijana zitakazofanyika Brazil Oktoba mwaka huu kutoka kundi hilo ni Nigeria na Angola, wakati kutoka Kundi B, Cameroon na Guinea zikifuzu fainali hizo huku Morocco na Senegal nazo zikiaga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mirambo, alisema kuwa matokeo hayo yamewahuzunisha pia benchi la ufundi na wachezaji, lakini hawana sababu ya kuyakataa kutokana na kuheshimu taratibu za soka.

Mirambo alisema wataangalia walipokosea na watafanyia marekebisho ili kuendelea kuwapa vijana wake nafasi ya kufunga zaidi.

"Naomba radhi kwa Watanzania wote, haikuwa matarajio yetu, lakini tunalazimika kukubaliana na kilichotokea, tulijiandaa vema ila tuseme haikuwa bahati yetu, tunarudi kuangalia tulipoishia ili kuwafundisha zaidi," alisema kocha huyo.

Naye nahodha wa timu hiyo, Maurice Abraham, alisema wameumizwa na matokeo, lakini hawajakata tamaa ya kuendelea kucheza mchezo huo.

Abrahamu alisema wataendelea kujifua na kuendelea na mashindano mengine yatakayotokea.

Mechi za nusu fainali zitapigwa keshokutwa, Jumatano wakati ya kutafuta mshindi wa tatu ikipigwa Jumamosi kabla ya ile ya fainali kuchezwa Jumapili.



Meneja Mauzo wa Kampuni ya Bia Tanzania (Tbl), Joseph Nicolous (wa pili kulia), akimkabidhi Kombe nahodha wa timu ya Girl Queens, Zubeda Mgunda, mara baada ya kuibuka Mabingwa wa Castle Africa 5s Bonanza lililofanyika Viwanja vya Leaders jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Katikati nyuma ya Kombe ni Balozi wa Castle Africa 5s Tanzania, Ivo Mapunda. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Girl Queens kuiwakilisha Tanzania Castle Africa 5s

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU soka ya Girl Queens yenye makazi yake mtaa wa Msimbazi Kariakoo jijini Dar es Salaam, imeibuka mabingwa wa Bonanza kubwa la Soka la Wanawake lililofanyika mwishoni mwa wiki katika Viwanja vya Leaders kwa udhamini wa Kampuni ya Bia nchini (TBL) kupitia bia yake ya Castle Lager.

Kwa kutwaa ubingwa huo, mbali na kuzawadiwa kombe, medali za dhahabu, pesa taslimu kiasi cha Sh. 900,000 na katoni ya bia ya Castle Lager, mabingwa hao wataiwakilisha nchi katika mashindano ya Caslte Africa 5s kwa Wanawake yanayotarajiwa kufanyika mwezi ujao jijini Dar es Salaam.

Girl Queens waliutwaa ubingwa kwa kuongoza baada ya kucheka na nyavu mara nyingi zaidi kwa kufunga mabao 12, wakifuatiwa na timu ya Msimbazi Queens (mabao tisa) ambayo ilishika nafasi ya pili na hivyo kuzawadiwa Sh. 600,000 huku Wema Queens ikishika nafasi ya tatu na kuibuka na Sh. 300,000.

Akizungumza na wachezaji, waandishi wa habari pamoja na wakazi wa jijini Dar es Salaam waliojitokeza kwenye Bonanza hilo, Meneja Mauzo wa TBL, Joseph Nicolous, alianza kwa kuwapongeza mabingwa Girl Queens kwa kutwaa ubingwa na kuwaomba zawadi walizozawadiwa zikawe chachu ya maandalizi mazuri ya kuiwakilisha nchi katika mashindano ya Castle Africa 5s kwa Wanawake yanayotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

Nicolous pia aliwapongeza washindi wa pili na tatu kwa ushindi pamoja na timu zote zilizoshiriki Bonanza hilo ambazo ni Chinga Queens kutoka Kariakoo, Siza Sisters (Kariakaoo), Tabata Queens (Tabata), Dragon (Mwananyamala), Bulyaga (Temeke), Mwangaza Queens (Temeke), Furaha Queens (Gerezani), Umoja Queens (Kidongo Chekundu), MRJ Queens (Mlandizi), Wema Dallas Queens (Mlandizi), Jupita (Buguruni Sukita), Mercury (Msimbazi), La Capilla na Santiago kutoka Mbagala.

Naye Balozi wa Bia ya Castle Africa 5s Tanzania, Ivo Mapunda aliishukuru Kampuni ya TBL kwa maandalizi na uratibu mzuri wa Bonanza ambao umetoa bingwa na mwakilishi wa mashindano ya Castle Africa 5s Wanawake yajayo, na kwamba anaamini Girl Queens itahakikisha ubingwa wa Afrika unabaki Tanzania.




## Ronaldo anuka rekodi Juve ikitwaa ubingwa

UKURASA 30




Richarlison akibinjuka na kuifungia Everton bao la kwanza wakati ikishinda 4-0 dhidi ya Manchester United kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Goodison Park jana. Mabao mengine yalifungwa na Gylfi Sigurdsson, Lucas Digne na Theo Walcott. **PICHA: MTANDAO**

# Aussems aonyesha anapokosea Zahera

## Ni baada ya Simba kukubali kichapo...

**Na Somoe Ng'itu**

HONGERA Kagera Sugar! Hayo ndio maneno aliyoanza kusema Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, baada ya timu yake kuchapwa mabao 2-1 na wenyeji wao katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa juzi katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

**Hali hiyo imekuwa tofauti na Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera ambaye amekua akinukuliwa kulalamika mara kwa mara juu ya waamuzi na ratiba ngumu kwa timu yake ambayo inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo.**

Na katika hilo ratiba ya Simba inaonyesha itakuwa ikicheza mechi moja baada ya siku mbili ama ambapo kesho itashuka tena dimbani kuivaa Alliance kabla ya Alhamisi kucheza dhidi ya KMC na Jumamosi kuvaana na Biashara United.

Akizungumza baada ya mechi hiyo juzi, Aussems alisema timu yake haikucheza vizuri katika kipindi cha kwanza ambacho Kagera Sugar ilifanikiwa kupata mabao mawili na iliporejea haikuweza kufanikiwa kuyarejesha.

Kocha huyo alisema hali hiyo iliwaweka katika nafasi ngumu na kusababisha kumaliza mchezo huo kwa kuacha pointi tatu kwenye uwanja huo wa Kaitaba.

"Dakika 45 za kwanza hatukucheza vizuri, tuliwaruhusu wenyeji watawale mchezo, lakini katika kipindi cha pili timu ilibadilika na kufanya mashambulizi, mpira ni dakika 90, ukicheza vema dakika 45 hazitoshi, tulifanikiwa kupata bao moja, kutoka nyuma ukiwa umefungwa mawili ni ngumu sana," alisema Aussems.

Naye nahodha wa Simba, John Bocco, alisema kuwa mechi hiyo ilikuwa ngumu na haikuwa nia ya wachezaji wa timu hiyo kupoteza mchezo huo.

"Haikuwa nia yetu kupoteza mechi hii, tulijituma sana lakini hatukufanikiwa kutumia nafasi zote tulizotengeneza, tunajipanga na mchezo ujao ili tuweze kupata ushindi," alisema mshambuliaji huyo.

Aliongeza licha ya kuwa na ratiba ngumu, bado watajipanga kupambana nao kwa malengo ya kushinda na hatimaye kutetea ubingwa wa ligi hiyo wanaoushikilia.

Kocha wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema kuwa walifanikiwa kupata ushindi dhidi ya Simba kutokana na kuingia katika kipindi cha pili wakiwa tofauti.

"Kipindi cha pili hatukuwa na kasi kwa sababu tulikuwa tunajilinda, tulikuwa tunacheza kwa tahadhari kwa sababu tulikuwa hatutaki Simba wapate bao, ndio maana tulikuwa tunapoozesha mpira, Simba ni timu kubwa yenye wachezaji wazuri kila idara na unapokuwa umewawahi, unahitaji kujilinda tu," Maxime alisema.

Aliongeza kuwa bado ligi hiyo ni ngumu kwao na hawako nafasi salama licha ya kufikisha pointi 39 na wanajipanga kurejeana na Simba katika mchezo wa mzunguko wa pili wa ligi hiyo.

Kwingineko, vinara wa ligi hiyo, Yanga kitarejea mazoezini kesho, Jumanne kwa ajili ya kujiandaa kuikabili Azam FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Aprili 29 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, alilimbia gazeti hili kuwa wanatarajia kufanya mazoezi kwa siku zisizopungua tatu na baadaye kuingia kambini ili kujiwinda na mchezo huo.

# Sevilla yathibitisha kuzivaa Simba, Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Sevilla FC inayoshiriki Ligi Kuu Hispania, La Liga, imethibitisha kumalizia maandalizi ya msimu mpya wa ligi kwa kucheza na moja ya klabu kongwe nchini kati ya Simba au Yanga itakapofanya ziara nchini.

Kampuni ya Kubashiri Matokeo Michezoni ya SportPesa kwa kushirikiana na La Liga ndiyo inafanikisha ziara hiyo ya kuileta Sevilla Tanzania kwa ajili ya ziara ya kimichezo inayokwenda kwa jina la 'SportPesa Laliga Challenge'.

Mchezo huo umepangwa kupigwa Mei 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam ambao utakuwa sehemu ya maandalizi ya Sevilla kujiandaa na msimu mpya wa ligi.

"La Liga imepanga kuwa karibu na mashabiki wake, hivyo ni nafasi ya kipekee kwa kila shabiki Mtanzania wa Sevilla kupata nafasi ya kuiona,"alisema Oscar Mayo ambaye ni mratibu wa La Liga.

Kwa upande wa Mkuu wa Utawala na Udhibiti wa Kampuni ya SportPesa Tanzania, Tarimba Abass alisema: "shukrani kubwa kwa Sevilla ya La Liga kwa kukubali kuja nchini katika ziara yao kufunga maandalizi ya msimu mpya wa ligi, wachezaji wetu watapata nafasi ya kuonyesha vipaji walivyokuwa navyo."

Katibu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao naye alisema: "Siyo jambo dogo kupata ugeni wa klabu kubwa kama Sevilla ambayo inashiriki ligi bora ya La Liga.

"Sevilla ina wachezaji 11 wanaocheza timu za taifa kutoka nchi mbalimbali ikiwamo Argentina, Hispania na Italia, hivyo kama TFF tunaahidi kushirikiana na SportPesa kuhakikisha maandalizi yote yanakwenda vizuri katika kuelekea mchezo huo."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002